# Adaiwa kujiua kwa sumu kisa ujumbe mapenzi simu ya mumewe

UKURASA 2




# DC atangazia vita kaya kwa ukosefu vyoo bora

UKURASA 3

UKURASA 21



# MAGUIRE AMPORA NAMBA VARANE


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 12, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • No. 0581492

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Muziki mnene magari shule janga kimaadili

UKURASA 2




UKURASA WA 17

## ISRAEL YADAIWA KUSHAMBULIA HOSPITALI GAZA

# Makonda ambana Aweso kero ya maji

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM

# Nyuma ya pazia wanawake wengi kupoteza ujauzito

UKURASA 4



MICHEZO YANGA YAONGOZA TAKWIMU ZOTE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Wananchi wakipitisha vyombo vya usafiri katika maji yaliotuama eneo la Makuti, Temeke jijini Dar es Salaam kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Muziki mnene mabasi ya shule janga lingine kimaadili, elimu

**Na Waandishi Wetu**

NI janga jipya. Ndivyo inavyoonekana sasa kutokana na magari mengi ya wanafunzi kuwa na muziki mnene huku watoto wakionekana kufurahia bila kujua madhara yake kimaadili na kielimu.

Hali hiyo inaendelea kushamiri kwenye mabasi hayo huku serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa na mwongozo unaokataza kucheza muziki usio na maadili katika mabasi ya shule.

Kutokana na hali hiyo, wataalamu wa saikolojia wanaonya kuwa sauti itokanayo na muziki hujirudia kichwani mwa mtoto, hivyo kuwa kikwazo katika ujifunzaji anapokuwa darasani.

Licha ya kuwapo kwa mwongozo huo na angalizo hilo la kitaalamu, Nipashe Jumapili imebaini kuwa, liko tatizo katika baadhi ya shule zenye mabasi ya wanafunzi kuwamo muziki mnene na wakati mwingine video zizisozingatia maadili na makuzi ya mtoto huchezwa.

Jijini Dodoma, mathalan kumeripotiwa na waandishi wetu kuwapo kwa changamoto hiyo kwa baadhi ya mabasi yanayobeba wanafunzi.

**WAZAZI NA WADAU**

Mkazi wa jiji hilo, Sarah Moses, mzazi mwenye mtoto anayetumia usafiri huo, anasimulia namna alivyobaini basi analopanda mtoto wake likiwa limefungulia muziki mnene.

"Siku moja gari la shule lilimfuata mtoto wangu nyumbani likiwa linapiga muziki kwa sauti ya juu na wimbo wenyewe ulikuwa wa kidunia (jina linahifadhiwa). Nilitoa taarifa kwa uongozi wa shule na walichukua hatua na sasa wanawawekea watoto katuni," alisema.

Christopher Dioniz, mkazi mwingine wa Dodoma, alisema kutoka na hali hiyo, anaishauri serikali kupitia kikosi cha usalama barabarani kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kudhibiti hali hiyo.

Alisema kama kuna ulazima wa basi la shule kuwa na TV na redio, basi watoto wawekewe frashi maalum zenye vipindi vya kujifunza masuala ya elimu au nyimbo zenye maadili.

Mkoani Dar es Salaam, baadhi ya wazazi wametaja kuwapo kwa changamoto hiyo inayochangia watoto kuimba nyimbo ambazo hazilingani na umri wao.

"Mtoto wa umri wa miaka mitano unakuta anaimba wimbo wa mapenzi tena wenye maneno makali ambayo hata wewe mtu mzima huwezi kuimba na anaucheza kwa hatua zote.

Ukimuuliza anakwambia anaona kwenye TV ya kwenye basi la shule, tunajenga kizazi cha aina gani?" anahoji John Stanslaus, mkazi wa Kinondoni.

Kilio hicho pia kimeripotiwa mkoani Kilimanjaro kwa mkazi wa Moshi Airport, ambaye hakupenda jina lake liandikwe, akisema endapo hatua hazitachukuliwa, mabasi hayo yataendelea kuwa kichaka cha watoto kujifunza vitu visivyofaa.

"Mtoto anaweza kuja nyumbani ana majeraha mwilini, unapouliza anakwambia aliumia ndani ya basi wakati wakicheza muziki. Ukimuuliza mwalimu anarusha mpira kwa dereva. Mzazi unabaki katikati hujui ufanye nini," alisema.

Sophia Everton, mzazi wa mmoja wa wanafunzi wanaoathirika na hali hiyo, aliomba serikali kama hakuna mwongozo basi utolewe na kama basi lina TV, zitumike kuweka vipindi vya kufundisha au kupiga nyimbo zenye maudhui yanayoendana na umri wa mtoto.

Mmoja wa madereva anayeendesha magari ya shule mkoani Kilimanjaro (jina linahifadhiwa), alisema: "Hayo yanaelezwa yote yapo, lakini kuna tabia za watu. Binafsi ninawalaumu wazazi hawawafuatilii watoto wao, wakiamini wakishalipa usafiri inatosha."

Mmiliki wa Shule za Kassa, mkoani Mwanza, Albert Kassa, alishauri wamiliki wa shule wenye magari yenye TV na redio kama watashindwa kudhibiti vyombo hivyo kwa kuweka vitu vyenye maadili, waviondoe kwa kuwa badala ya mtoto kuimba nyimbo nzuri wanaimba za mahaba.

"Siku moja nikiwa kwenye mahafali, watoto waliimba wimbo wa kawaida (wakidunia), nilishangaa mtoto mmoja anacheza staili ambayo sijawahi kuiona, nikasema amejifunzia wapi?" alihoji.

Alilitaka pia Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) kuangalia nyimbo za wasanii na kama zitaonekana hazina maadili zisiruhusiwe kupigwa katika vyombo vya habari.

Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Ukerewe, Mwanza, Rasul Amiri, alitaka wazazi kila mmoja kuchukua jukumu la kumsimamia mtoto wake na shule zipewe elimu kwa kukumbushwa kuzingatia maadili.

"Ni kweli athari ni nyingi, nidhamu haipo, watoto wanakuwa na tabia za mtaani zaidi. Hii inachangia ufaulu wa mtoto kutokuwa mzuri, anajikita katika mambo ya kidunia zaidi hasa muziki," alisema.

**MWANASAIKOLOJIA AFUNGUKA**

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma ambaye pia ni mtaalamu wa masuala ya saikolojia, Mutapha Rajabu, alisema kwa kawaida sauti ya muziki huwa na tabia ya kujirudia kichwani, hivyo mtoto anaposikiliza nyimbo itamwathiri hata awapo darasani.

"Mtoto anaathirika kutokana na sauti za muziki ya kidunia inayopigwa katika magari ya shule kwa kuwa, sauti zina tabia ya kujirudia kichwani na anachokibeba leo mtoto hicho atakitumia katika miaka yote hakitoki mapema," alisema.

Alisisitiza kuwa kichwa cha mtoto ni sawa na CD tupu ambayo inarekodi vitu vizuri na vibaya, hivyo anaposikiliza anashindwa kujifunza vizuri mambo ya darasani kutokana na kichwa kujaza sauti za muziki.

**WAZIRI ANENA**

Nipashe ilipomtafuta Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, ili kufahamu kama wizara ina mwongozo unaokataza kucheza muziki katika mabasi hayo, alisema mwongozo huo upo na ulitolewa mapema mwaka huu.

"Mwongozo huu unakataza kucheza muziki usio na maadili katika mabasi ya shule na umetoka mwaka huu," alisema.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini, Ramadhani Ng'anzi, katika mahojiano maalum na Nipashe alikiri miongoni mwa makosa ambayo hukutana nayo wakati wa ukaguzi wa mabasi ya wanafunzi ni madereva kufungua muziki mnene.

"Katika ukaguzi huo baadhi ya mikoa kama Shinyanga kuna watu walikamatwa, Mbeya walifikishwa mahakamani, Kigamboni (Dar es Salaam) wamiliki wa shule walikamatwa na kuhojiwa na magari yalikaguliwa upya na kung'olewa vifaa kama hivyo," alisema.

Kamanda Ng'anzi amewashauri wazazi pamoja na kulipa gharama za usafiri, wahakikishe usalama wa watoto wao unakuwapo na wanapoona changamoto wapige simu yake namba 0656 111 444 na wenye shule ametaka waajiri watu wenye maadili.

**IMEANDALIWA na Romana Mallya (DAR) Mary Mosha (MOSHI), Paul Mabeja, (DODOMA) na Neema Emmanuel MWANZA**

## Adaiwa kujiua kwa sumu kisa ujumbe mapenzi simu ya mume

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKAZI wa Kitongoji cha Matarawe, Kijiji cha Marungu Tingi, Nyasa mkoani Ruvuma, Marietha Sangana, amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Misheni ya Maguu wilayani Mbinga baada ya kunywa sumu ya kuulia wadudu.

Sangama anadaiwa kuchukua uamuzi huo wa kunywa sumu ya kuulia wadudu kwenye mahindi baada ya kukuta ujumbe wa mapenzi kwenye simu ya mume wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Marco Chilya, alisema jana alipozungumza na Nipashe kwa simu kwamba tukio hilo lilitokea Novemba 9, mwaka huu, katika kijiji cha Marungu wilayani Nyasa.

Alisema kabla ya siku ya tukio hilo, Sangana akiwa nyumbani kwake, ghafla aliiona simu ya mume wake ikiwa mezani ambayo alikuwa ameisahau wakati akienda shambani.

Kamanda Chilya alisema siku hiyo mume wa Sangama alikuwa ameenda shambani lakini kwa bahati mbaya alikuwa amesahau kuichukua simu yake ndipo mke wake alipata nafasi ya kuanza kusoma ujumbe mbalimbali kwenye mtandao wa WhatsApp. Alisema akiwa anasoma ujumbe, ghafla aliona ujumbe wa mapenzi na akafanikiwa kuona mawasiliano kati ya mume wake na mwanamke mwingine (mchepuko).

Alisema kutokana na hatua hiyo, Sangama alishindwa kuvumilia na kuamua kuchukua dawa ya kuulia wadudu aina ya ACTERIC iliyoandaliwa kwa ajili ya kuweka kwenye mahindi na kuinywa.

"Baada ya kitendo hicho kutokea, majirani wanaoishi na Sangama waligundua kuwa kuna sauti ya mtu ambaye alikuwa anasema 'naomba mnisaidie' ndipo majirani walipofika na kumkuta akiwa taabani.

"Walipomuuliza aliwaeleza kuwa amekunywa dawa ya kuulia wadudu ndipo walipomchukua na kumkimbiza katika Hospitali ya Misheni ya Maguu wilayani Mbinga ambako baadaye Novemba 10 (juzi) alifariki dunia," alisema.

Kamanda Chilya alisema Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma limeshaanza kufanya uchunguzi ikiwa ni pamoja na askari wa upelelezi wilayani Nyasa kwenda kwenye eneo la tukio.

Aidha, Chilya alisema polisi wanamshikilia mume wa marehemu na mchepuko ambao majina yao yamehifadhiwa kwa mahojiano zaidi.

## HABARI KITAIFA



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, akiwasili kwa usafiri wa farasi kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika stendi ya mabasi ya zamani wilayani Chato, mkoani Geita juzi. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Makonda ambana Aweso kero ya maji

**Na Beatrice Shayo,** GEITA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameomba kupewa wiki tatu kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji kwa wananchi wa Katoro na Buseresere mkoani Geita baada ya kulalamika kuikosa huduma hiyo kwa muda.

Wananchi hao walimlalamikia Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, kuwa wanakabiliwa na tatizo la maji, barabara, umeme na taa za barabarani wakati aliposimamisha msafara katika mji mdogo wa Katoro wilayani Geita.

Baada ya kusikiliza kero za wananchi, Makonda aliwajulisha wananchi kuwa changamoto kubwa katika maeneo hayo ni maji na chama kinamwelekeza Waziri Aweso kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Makonda alimpigia simu Aweso na kuweka sauti ili wananchi kumsikiliza majibu yake.

"Waziri atuambie kama hela ipo kwa nini maji hayapo? Mheshimiwa Waziri nipo hapa Katoro, Buseresere, Busanda na kona zake zote ndani ya wilaya ya Chato na Geita. Hebu niambie fedha za maji zipo? Na kama zipo lini mradi wa maji unaanza kufanyiwa kazi na wananchi kupata maji katika hayo maeneo?" alihoji.

Aweso akitoa majibu kwa njia ya simu alisema eneo hilo alishalitembelea na moja ya changamoto kubwa ni maji tayari wameanza kulifanyia kazi kuna mradi wa maji wenye gharama ya Sh. bilioni sita na kwa sasa umefikia asilimia 92 na hivi karibuni mbunge wa jimbo hilo alimfuata kumwomba Sh. milioni 500 na tayari zimeidhinishwa.

"Mradi huo ambao upo asilimia 92 naomba unipe wiki tatu wananchi hao wanaenda kunywa maji safi na salama kama chama kilivyotuelekeza kuhakikisha maji yanapatikana kwa wananchi," alisema Aweso.

Aweso pia alisema wametoa maelekezo mahususi hasa eneo la kanda ya ziwa kwamba ziwa Victoria litumike kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji kwa mkoa wa Geita na maeneo mengine.

Alisema wana mradi wa miji 28 wamepewa maelekezo itakapofika mwaka 2025 wawe wamefikisha asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mijini na eneo la Geita wana asilimia 75.

"Eneo la Chato kuna mradi wa maji zaidi ya Sh. bilioni 38 na mkandarasi yupo anaendelea na kazi lengo ni kuhakikisha tunatatua tatizo la maji kwa ufupi mkoa wa Geita una vijiji 489 na vilivyofikiwa na maji ni vijiji 333 mkakati tuliopewa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha vijiji vinapata huduma ya majisafi na salama," alisema Aweso.

Baada ya kutoa maelezo hayo, Makonda alisema wana deni kwa wananchi kwa sababu ni wasimamizi wa ilani ya uchaguzi ya chama, watekelezaji na kuwataka wananchi kusubiri maji ndani ya wiki tatu watapatiwa na yeye atakuwa mfuatiliaji wa ahadi hiyo iliyotolewa.

Makonda alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kilichobaki ni msukumo wa kupeleka maendeleo kwa wananchi na wao kazi yao kubwa ni kufuatilia ili kero za wananchi zitatuliwe.

Awali, Makonda alisema eneo hilo lina matukio ya uhalifu na wanafanya matukio hayo inawezekana wanafahamika chama kingetamani kuona wanatoa ushirikiano mzuri kuanzia ngazi ya kijiji, kata, wilaya hadi mkoa kuhakikisha wanaochafua ukanda huo kwa kufanya uhalifu wanabainishwa na hatua stahiki kuchukuliwa.

"Lengo ni kuhakikisha Katoro, Busanda na wilaya yetu ya Geita inabaki kuwa sehemu tulivu ya amani na mshikamano kwa wananchi kufanya shughuli za maendeleo," alisema Makonda.

Pia Makonda ametoa maelekezo kwa wale wote ambao wamekamatwa mikaa yao na pikipiki kuhakikisha wanarudishiwa wananchi hao.

"Hizi sheria jamani zinanishangaza kuna ndugu yangu mmoja amepigwa faini ya Sh. 300,000 kwa ajili ya mkaa haijatosha wamemtaka alipe Sh. 500,000 kwa ajili ya kuikomboa pikipiki yake yaani pikipiki yake utasema ameenda kuikopa ni jambo la ajabu sana," alisema Makonda.

Makonda aliagiza kinamama wanaouza mkaa kwenye vibaraza vyao wasinyanyaswe na hiyo ni kauli ya chama.

# DC atangazia vita kaya ukosefu vyoo bora

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, ametoa siku 10 kwa kila kaya kuwa na choo cha kisasa na kuonya kuwa ambayo itabainika haina hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na watumishi wa wilaya hiyo na kuwaagiza wenyeviti na watendaji wa vijiji, watendaji wa kata na maofisa tarafa kusimamia agizo hilo ili kukabiliana na ugonjwa wa mlipuko wa homa ya kutapika na kuharisha katika kipindi hiki cha mvua.

"Hakikisheni kaya zote wilayani Mkalama zinakuwa na vyoo na kutoa siku 10 kwa kaya ambazo hazina vyoo kujenga na kuwachukulia hatua kali za kisheria watakaokiuka agizo hili," alisema.

Machali alisema ugonjwa wa kipindupindu unasababishwa na uchafu wa mazingira kutokana na kaya nyingi wilayani hapa kukosa vyoo bora, hivyo njia pekee ya kuepukana na ugonjwa huo ni kila kaya iwe na choo bora.

Alisema kuanzia sasa watendaji katika vijiji na kata zote waitishe mikutano ya hadhara katika maeneo yao ili kuwapa elimu wananchi juu ya usafi wa mazingira pamoja na kuwa na vyoo bora.

"Maelekezo yangu ni kwamba nendeni kwenye maeneo yenu. Wewe mwenyekiti wa kijiji, mtendaji wa kijiji, kata mkahakikishe ndani ya siku 10 kila kaya inakuwa na choo bora. Natoa maelekezo kuwachukulia hatua watakaopuuza agizo hili," alisisitiza.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwataka viongozi wa dini wanapokuwa kwenye nyumba za ibada kutoa elimu kwa waumini wao kuhusu hatari ya kuwapo kwa maambukizi ya kipindupindu, hivyo tahadhari zote za kiafya za kuzuia maambukizi hayo kuenea katika maeneo mengine zianze kuchukuliwa.

Aliongeza kuwa maeneo yote ya taasisi za umma, mashirika ya dini, masoko, shule, stendi ya mabasi, nyumba za ibada na kwenye mikusanyiko kuwapo vifaa vya kunawia mikono zikiwamo sabuni na vitakasa mikono na wananchi kuacha kusalimiana kwa kutumia mikono ili kuzuia maambukizi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Machali alimwagiza Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mkalama kuchukua sampuli za maji na kutibu visima virefu na vifupi ndani ya wilaya ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa kutapika na kuharisha.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD , SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 22/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | 1.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.59847 KIWANJA NA.2009 KITALU "D" | 1.LAMECK JOHN RUGIGA 2.CRISPIN PATRICK KAPILIMBA | 1.MBEZI MSHIKAMANO 2.SINZA | 21/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL SANGA | ITETE KYELA MBEYA | 20/11/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 23/11/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | KELVIN COSTA LEONARD | PAGALE LA NYUMBA | ANTONETA HENERY KOSIMAS | MKONZE CHINYIKA | 27/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | BAHATI NASSON SAMILA | NYUMBA | BAHATI NASSON SAMILA | MBUYUNI KIZOTA | 27/11/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | ABUSHIRI HASANI MSONGO | NYUMBA | ABUSHIRI H. MSONGO | IHUMWA-DODOMA | 28/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | PETER ODHIAMBO BOAZ | NYUMBA | PETER ODHIAMBO BOAZ | BAHI | 29/11/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | IMAN SAJENI SANGA | NYUMBA | IMAN SAJENI SANGA | CHIMALAA NTYUKA | 28/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | ARONI STEPHANO GUNDA | NYUMBA | SHEILA MNENEGWA PETER | KISASA-DODOMA | 28/11/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | JOYCE STEVEN MSOFU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MONICA THADAYO CHISUMUNI | NG'HONG'HONA | 29/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja , Shamba au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0745707008/0787129539/0765999000/0759282344/0754497396**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

**217710002**

RIPOTI MAALUM

# Nyuma ya pazia wengi kupoteza ujauzito Dar

Na Christina Mwakangale

KATIKA kila wanawake 100 wanaoshika ujauzito Dar es Salaam, 23 unaharibika, utafiti wa serikali umebaini.

Mnamo Oktoba 28 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua ripoti ya utafiti huo uliopewa jina la Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Mwaka 2022, ikionesha asilimia 23 ya wanawake wanaoshika ujauzito Dar es Salaam unaharibika.

Hata hivyo, serikali haijataja sababu mahususi zinazochangia tatizo hilo katika ripoti ya utafiti wake huo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Kuangazia yaliyojificha juu ya tatizo hilo, mwandishi wa habari hizi amedokezwa na wataalamu wa afya ya uzazi kwamba msongo wa mawazo, uchovu wa mwili na mazingira ya shughuli zilizotawaliwa na mikikimikiki ya miji mikubwa, ikiwamo Dar es Salaam, ni sehemu ya vyanzo vya ujauzito kuharibika.

Aisha... (jina la pili tunalo) ni mamalishe katika stendi ya daladala Feri (Kivukoni), jijini Dar es Salaam. Saa 11 alfajiri wiki iliyopita, alikutana na mwandishi katika basi dogo linalofanya safari kati ya Gongo la Mboto na Msasani.

Mkononi alibeba kikapu kilichofunikwa na mifuko kadhaa kuficha kilichomo ndani. Aisha, katika mazungumzo na mwandishi, anafafanua ratiba yake ya wiki kuwa kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, hurejea nyumbani kwake kati ya saa tatu na saa nne usiku.

“Ninakumbuka mwaka 2016, ilikuwa Jumamosi. Ni siku ambayo huwa ninafanya shughuli za usafi nyumbani kwangu, nikimaliza ninakwenda kwa Mama Chau - msusi wa nywele za mkono (maarufu twende kilioni) jirani na ninapoishi.

“Kutoka kwangu na kwake ni kama hatua 20 hivi. Ghafla nikajihisi tofauti pale nilipoketi chini wakati wa kusukwa. Pembeni walikuwapo wanawake wawili, wakiwa kwenye foleni ya kusukwa.

“Sikutaka kuonesha dalili kwamba kuna kitu nimehisi, tuliendelea na maongezi, si unajua mkikutana kinamama wawili watatu sehemu moja... maongezi yenu huwa yanaendana.

“Zikiwa zimesalia ‘nywele mbili’ (mistari miwili katika mtindo wa twende kilioni) kusukwa, nilimwomba msusi kwenda msalani, alinielekeza. Hiyo ilikuwa ni mbinu yangu kwenda kuthibitisha nilichokuwa ninajihisi.

“Nilipoinuka, mambo yalikuwa yameharibika... nilipewa kanga na msusi kujisitiri hadi maliwato, huko nilichukua kama dakika 15 hivi. Mimba imetoka! Sikuamini!,” alisema.



Mjasiriamali huyo anabainisha ujauzito uliharibika katika wiki la 10, yaani miezi miwili na nusu. Saa chache baadaye alikumbwa na maumivu ya tumbo mithili ya uchungu wa kujifungua.

“Nilirudi nyumbani kwangu kujiandaa kwenda hospitalini nilikopewa huduma ya kwanza na baadaye... (alitamka neno lenye fasili ya matibabu yanayotolewa kwa kinamama ambao ujauzito umeharibika).

“Ninafikiri purukshani za usafiri wa Dar zilichangia ujauzito wangu kutoka,” anasema Aisha (30), mkazi wa Madafu, Ukonga jijini Dar es Salaam.

Anabainisha kuwa sasa ni ‘mama kijacho’ tena. Ujauzito una miezi sita. Licha ya kufahamu fika kwamba purukshani za usafiri anaotumia kwenda kazini Kivukoni ni hatari kwa usalama wa kiumbe kilichomo tumboni, analazimika kuutumia kutokana na hali yake kuwa duni kiuchumi.

“Mume wangu hana kipato kikubwa, hivyo tunasaidiana kutafuta mahitaji ya watoto wetu wawili; mmoja anasoma darasa la kwanza na mwingine la awali. Nikibaki nyumbani bila kufanya kazi, maana yake tutakosa mahitaji ya watoto,” anasema.

**WATAALAMU WANENA**

Wataalamu wa afya ya uzazi waliozungumza na mwandishi, wanabainisha kuwa mazingira ya miji mikubwa, iliyo na pilika nyingi za kiuchumi, ikiwamo Dar es Salaam, yanaweza kuwa vyanzo vya ujauzito kuharibika.

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Hillary Kizwi, anataja vyanzo vingine vya ujauzito kuharibika ni pamoja na maambukizi, msongo wa mawazo na uchovu.

Dk. Kizwi anafafanua kitalaamu kuwa ujauzito uliokamilika, unakuwa na umri wa kuanzia wiki 37 hadi 38. Kipindi hicho nacho kimegawanywa katika makundi matatu; miezi mitatu ya mwanzo, miezi sita na miezi tisa.

“Kwa ujauzito ambao umeharibika ni uliotoka ukiwa chini ya wiki 28. Kuna mmoja ambaye unaharibika mapema zaidi, mwingine baadaye wakati kiumbe kimeanza kuwa na uhai,” anafafanua bingwa huyo.

Dk. Kizwi anabainisha maambukizi katika mifumo ya uzazi, mkojo na upumuaji yanaweza kusababisha ujauzito kuharibika, pia maambukizi katika sehemu yoyote ya mwili yanaweza kuchangia tatizo hilo.

Kiumbe kilichomo tumboni kinapokuwa na umbile lisilostahili , Dk. Kizwi anasema ujauzito wake utaharibika mapema, mara nyingi ni chini ya miezi mitatu.

“Sababu nyingine ni matatizo ya kimaumbile, yaani shingo ya uzazi inakuwa inafunguka pamoja na upungufu wa homoni za kulinda ujauzito (progesterones).

“Chanzo kingine ni makundi tofauti ya damu yatokanayo na wazazi wote wawili. Utakuta baba ni AB+ au mama ni O- ama B- na baba pengine ni B+. Sasa hawa wazazi utakuta katika ujauzito mama atatengeneza ‘antibodies’(kingamwili) bila kujijua na kuharibu mimba.

“Sababu zingine ni mazingira yanaweza kuchangia ujauzito kuharibika kama vile kuchoka, kufanya kazi ngumu. Hii inaweza kusababisha mtu kutengeneza ‘fatigue’ (uchovu) kama Dar es Salaam, mtu anakuwa na pilika nyingi kimaisha,” anasema.

Bingwa huyo anashauri wajawazito kutofanya kazi ngumu ma kufuata miongozo ya wataalamu wa afya ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kliniki ambako mbali na huduma zingine, watapimwa viwango vya homoni, ili kama viko chini, wapewe dawa kuvipandisha.

Bingwa huyo anaonya kinamama wanaopuuza mahudhurio ya kliniki wakati wa ujauzito kwa kigezo kwamba wana uzoefu na ujauzito. Ni hatari kwao na viumbe tumboni.

“Chini ya miezi mitatu ni kipindi kilicho na uwezekano mkubwa kuharibika ujauzito kutokana na homoni kutokaa sawa,” anahadharisha Dk. Kizwi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Nicodem Komba, pia anataja sababu kadhaa zinazoathiri ujauzito, zikiongozwa na matatizo ya chembe uzi (chromosomal abnormalities).

Kama ilivyoelezwa na mtangulizi wake Dk. Kizwi, Komba anataja maambukizi katika mifumo ya mkojo na upumuaji, matatizo ya kimaumbile, mfuko wa uzazi, matatizo ya homoni na magonjwa ya kudumu kwa mama yanachangia ujauzito kuharibika.

“Kuna sababu zingine kama vile ajali au mjamzito kupigwa, msongo wa mawazo na kuwa katika mazingira ya sumu za kuulia wadudu, dawa au kemikali za viwandani na migodini, uvutaji sigara, unywaji pombe, ujauzito katika umri mkubwa na historia ya mimba kuharibika,” anafafanua.

Kuhusu hali ya maisha na mazingira ya Dar es Salaam, Komba anasema: “Dar es Salaam labda kwa sababu ina idadi kubwa ya watu, kitu ambacho hupelekea pia kuwapo kwa idadi kubwa ya takwimu kitaifa mimba kuharibika.

“Lakini sababu nyingine ya kitakwimu kama ilivyoainishwa na ripoti hii, inaonyesha kwamba, maeneo ya mjini ndio yanaongoza kwa asilimia 13 ya utokaji mimba kitaifa kulinganishwa na maeneo ya vijijini ambayo ni asilimia sita.

“Kliniki ni muhimili muhimu sana katika kukuza na kuendeleza afya ya mama na mtoto na hatimaye taifa kwa ujumla. Husaidia kubaini maendeleo ya ukuaji wa mtoto, viashiria vya dalili za hatari kwa mjamzito na ushauri mahususi kwa mjamzito katika kipindi cha ujauzito na baada ya kujifungua,” anasema.

Anaeleza kuwa mjamzito anapaswa kuhudhuria kliniki kila mwezi, walau mara nane katika kipindi chote cha ujauzito. Hatari ya ujauzito kuharibika iko zaidi katika kipindi cha chini ya miezi mitatu ya mwanzo.

“Hatua za awali ambazo mkunga anatakiwa kuchukua mara akutanapo na mteja ambaye mimba imeharibika ni kumchunguza kwa haraka mteja kama ana tatizo lolote amabalo linahitaji matibabu ya haraka.

“Kutoka damu nyingi, kutopumua vizuri au kuzirai ni vitu ambavyo huchukuliwa kama dharura ili kuokoa maisha ya mama.

“Na kila mkunga anatakiwa kuwa na uwezo wa kubaini hivi viashiria vya hatari maana ndio huchangia kwa kiwango kikubwa kwenye vifo vitokanavyo na uzazi kwa nchi zetu zinazoendelea,” Komba anasema na kukumbusha kuwa TAMA ina jukumu la kuhakikisha usalama katika uzazi nchini. Ina wanachama hai 5,724.

**RIPOTI YA UTAFITI**

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 iliyozinduliwa na Rais Samia mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu, inabainisha asilimia 23 ya wanawake wanaobeba ujauzito mkoani Dar es Salaam unaharibika. Ni kiwango cha juu kuliko mikoa yote huku kiwasngo cha chini zaidi (chini ya asilimia moja) kikiwa Mkoa wa Rukwa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, utafiti huo ulihusisha wanawake 15,254 wenye umri wa miaka 15-49 kutoka kaya 15,705 zilizochaguliwa. Pia ulihusisha wanaume 5,763 wenye umri wa miaka 15-49 kutoka katika nusu ya kaya zilizochaguliwa.

Taarifa za ujauzito kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 kwa kipindi cha miaka mitatu kabla ya utafiti huo, zimeonesha katika ripoti ya utafiti huo kuwa asilimia 90 ya walijifungua watoto hai na asilimia 10 walipoteza ujauzito.

“Kati ya wanawake waliopoteza ujauzito, asilimia nane mimba zao ziliharibika, asilimia mbili ‘watoto wafu’ (siyo riziki) na asilimia chini ya moja walitoa mimba na asilimia 23 ya mimba (ujauzito) katika Mkoa wa Dar es Salaam ziliharibika.

“Hiki ni kiwango kikubwa kuliko mkoa mwingine wowote na kiwango cha chini zaidi (chini ya asilimia moja) kilikuwa Mkoa wa Rukwa,” inabainishwa katika ripoti hiyo ya utafiti wa NBS.

Ripoti hiyo pia inabainisha wanawake wengi walioolewa Tanzania Bara wanatumia njia za kisasa za uzazi wa mpango kulinganishwa na wale wa Tanzania Zanzibar (asilimia 32 kwa asilimia 17 mtawalia) huku wanawake wengi walioolewa wanaoishi mijini hutumia njia ya kisasa zaidi (asilimia 35) kulinganisha na vijijini (asilimia 29). Matumizi ya njia hizi ni makubwa kwa Mkoa wa Njombe (asilimia 56).



Ummy Mwalimu

## HABARI KITAIFA




Kaimu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (kushoto), akimpongeza mmoja wa wahitimu wakati wa mahafali ya 58 ya chuo hicho, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Muswada wapendekeza kuvibana vyama vya siasa ukiukaji sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 umependekeza masuala mbalimbali ikiwamo kuvibana vyama vya siasa vinavyokiuka sheria ikiwamo matumizi ya lugha za matusi.

Sambamba na hilo, muswada huo unapendeleza kuweka adhabu kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya uamuzi ndani ya chama husika.

Mapendekezo hayo yaliwasilishwa bungeni juzi na serikali na kifungu cha 6C cha muswada huo, kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka adhabu hiyo ili kukomesha vitendo vya watu wasio raia kuingilia katika uamuzi wa vyama vya siasa kwa kuwa kwa sasa sheria inaweka katazo lakini hakuna adhabu.

Aidha, kifungu hicho kinapendekeza ili kuboresha utaratibu wa uchukuaji wa hatua za kinidhamu ndani ya chama cha siasa kwa kuzuia mtu ambaye alishiriki katika kufanya uamuzi wa awali dhidi ya mwanachama, kushiriki katika kusikiliza rufani dhidi ya uamuzi huo.

Pia kifungu cha tisa kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa kwa chama cha siasa kuwasilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda ili kumpa msajili fursa ya kujiridhisha endapo kanuni hizo zimezingatia masharti ya sheria.

Kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kukinyima chama cha siasa sifa za kusajiliwa, endapo katiba na kanuni zake zinaruhusu matumizi ya lugha inayoweza kuhatarisha usalama wa nchi. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinavyosajiliwa ni vile vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali kwa maslahi mapana ya nchi.

Kadhalika, kifungu kipya cha 10C kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha nyaraka ambazo chama cha siasa kinapaswa kuwa nazo wakati wote.

Miongoni mwa nyaraka hizo ni sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalumu, kanuni za fedha na usimamizi wa mali na kanuni za uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi wa chama.

Marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha chama cha siasa kinaendeshwa kwa kuzingatia misingi na kanuni ilizojiwekea.

Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha kuwa maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322. Lengo la marekebisho hayo ni kuwianisha masharti ya kifungu cha 11 na masharti ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ambayo imeainisha utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano.

Kifungu cha 11A kinarekebishwa ili kuviruhusu vyama kushirikiana hata wakati wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika sheria.

Kifungu cha 13A kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa pale anapogundua kuwa mtu mwingine ametenda kosa au anakusudia kutenda kosa lolote chini ya sheria.

Lengo la marekebisho hayo ni kuzuia utendaji wa makosa na kuhakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya mtu anayekiuka masharti ya sheria.

Pamoja na hayo, kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka takwa kuwa mgawanyo wa ruzuku utafanywa kwa kuzingatia pia, matokeo ya uchaguzi mdogo.

Lengo la marekebisho hayo ni kuruhusu fedha za ruzuku kugawanywa kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika, badala ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama kilipata wakati wa uchaguzi mkuu pekee.

# Wadau kunolewa usalama mabwawa tope sumu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU na wamiliki wa migodi ya madini, wanatarajiwa kunolewa kuhusu ufuatiliaji wa usalama wa mabwawa ya tope sumu na mabwawa ya maji ya kawaida.

Mafunzo hayo maalum yalizinduliwa jana na yanatarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 28 hadi 30, mwaka huu jijini Mwanza. Pia yataambatana na mafunzo kwa vitendo katika mgodi wa dhahabu wa Bulyanhuli, Kahama mkoani Mwanza.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi huo jijini hapa, Mwenyekiti wa Chemba ya Madini Tanzania (TCM), Mhandisi Philbert Rweyemamu, alisemaa mafunzo hayo ambayo ni ya kwanza kufanyika nchini, yanatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa kiusalama katika migodi na mabwawa hayo.

Mafunzo hayo, kwa mujibu wa Rweyemamu, yatasimamiwa na TCM kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kupitia Idara ya Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji. Kwa mujibu wa Mhandisi Rweyemamu, mafunzo hayo ni mahususi kwa wadau na wafanyakazi wanaosimamia mabwawa ya tope sumu migodini na mabwawa ya maji, wataalamu wa usimamizi wa mazingira, maofisa mazingira wa wilaya kwenye maeneo ya migodi mikubwa na wasimamizi wa migodi.

Alisema wamejipanga kuendesha mafunzo hayo kwa lengo la kuwaelimisha wadau kuhusu teknolojia za kisasa zilizopo na kuwapa uelewa wa pamoja na fursa kuhusu ufuatiliaji wa usalama wa mabwawa hayo ya tope sumu na mabwawa ya maji ya kawaida.

"Usalama wa mabwawa hayo ni muhimu ili kuchukua hatua mapema kabla maafa hayajatokea.

Tunaamini kuwa maarifa yatakayopatikana kutoka kwenye warsha hii yatawaongezea wasimamizi wa sheria na wamiliki wa mabwawa uwezo katika kusimamia usalama, hivyo kupunguza uwezekano wa kutokea ajali zinazoweza kuepukika," alisema Mhandisi Rweyemamu.

Pia alisema mafunzo hayo ni fursa kwa wadau wote katika sekta ya madini na wa usimamizi wa rasilimali za maji na kwamba yanatarajia kukidhi matakwa ya sheria, hasa katika kuangalia vipengele muhimu vya usalama, udhibiti wa vihatarishi kuhakiki usanifu wa mabwawa na taratibu za tahadhari za mapema.

Mbali na wadau wa hapa nchini, alisema mafunzo hayo yatawakutanisha wataalamu kutoka kampuni ya OSIMO Technical (PTY) Limited ya Afrika Kusini na wengine kutoka Hispania.

Msimamizi wa Mabwawa kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Edward Malale, alisema kwa kutambua umuhimu wa usalama wa mabwawa kwa kulinda mazingira, wananchi na mali zao, TCM imekubali kushirikiana na serikali kupitia wizara hiyo kuhakikisha mabwawa ya maji tope sumu yanaendelea kuwa salama.

# Mbunge ataka vivutio uwekezaji vituo gesi asilia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na mwongozo wa maandalizi ya bajeti kwa mwaka 2024/25 huku Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, akishauri serikali itoe vivutio maalum kwa wawekezaji wanaotaka kujenga vituo vya kujazia gesi asilia.

Akichangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024/25 bungeni, Chikota alisema kwa sasa vituo hivyo viko vinne nchini huku zaidi ya kampuni 30 zikiwa zimeomba.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vyema kuwa na vivutio maalum ili kuongeza upatikanaji wa gesi hiyo itakayovutia wamiliki wa vyombo vya moto kubadili kutoka kwenye mafuta kwenda kwenye gesi.

"Tuwe na vivutio ili kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuwe na vituo vya gesi na maeneo mengine, tutoe punguzo maalum ili wawekezaji wajikite kwenye eneo hili," alisema.

Kuhusu usambazaji wa gesi viwandani na majumbani, Chikota alisema pamoja na kazi inayofanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) lakini haipewi fedha za kutosha.

"Naomba mpango ujielekeze kutoa fedha za kutosha ili usambazaji huu sasa uende kwenye mikoa yote isiwe Mtwara, Lindi na Dar es Salaam," alisema.

Aidha, alipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi inayofanya kwenye gesi asilia huku akishauri shughuli za mradi wa gesi asilia zifanyike kwenye eneo husika.

"Likong'o iko Manispaa ya Lindi si busara shughuli hizi zikaendelea kufanyika Dar es Salaam na Arusha wakati eneo la mradi lipo naomba sasa shughuli za LNG zihamie eneo husika, kuhusu vituo vya kujazia gesi vipo vichache," alisema.

Kadhalika, mbunge huyo alishauri katika sera ya elimu ya mwaka 2014 toleo la 2023, serikali ijielekeze katika ugharamiaji kwa kuwa inakwenda kubadili uendeshaji na usimamizi wa elimu.

"Kuanzia mwakani tunaanza kutekeleza mtaala mpya inamaana mtihani wa darasa la saba 2027 hautakuwapo kutakuwa na mtihani wa tathmini, takwimu zilizopo wanafunzi takribani asilimia 25 hawaendelei na kidato cha kwanza, hivyo tutakavyokuwa tunafanya tathmini wanafunzi wote wataingia kidato cha kwanza," alisema.

Alisema kutakuwa na mahitaji mapya ikiwamo madarasa, walimu, vyoo na kwamba inakadiriwa kuhitajika madarasa ya ziada 8733, vyoo 17,467 na kusisitiza lazima mpango ujikite katika kutafuta fedha za kugharamia mfumo mpya wa elimu.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inastahili pongezi miswada mabadiliko sheria

**SERIKALI** juzi iliwasilisha bungeni miswada minne ikiwamo mitatu inayopendekeza mabadiliko ya sheria katika masuala ya kisiasa na muundo mpya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mingine ni ya Mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi na Msajili ya Vyama vya Siasa.

Sambamba na miswada hiyo, serikali pia iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023 ambao pamoja mambo mengine unapendekeza kuwapo kwa utaratibu wa ushindani katika kupata majina ya wakuu wa mashirika ya umma ambayo yanamilikiwa kwa asilimia 100 na serikali. Miswada yote hiyo ilisomwa kwa mara ya kwanza huku ikisubiri kusomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa na wabunge kabla ya kupitishwa na hatimaye kutiwa saini na Rais ili kuwa sheria kamili.

Katika muswada wa sheria ya masuala ya siasa, inapendekezwa kuwa katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), mwenyekiti, makamu mwenyekiti na mkurugenzi wa uchaguzi wateuliwe na Rais lakini wajumbe, ambao ni makamishna wa tume hiyo, waombe na kufanyiwa usaili kabla ya kupitishwa kutumikia nafasi hizo.

Aidha, katika uchaguzi wa Rais, Madiwani, Wabunge na viongozi wa serikali za mitaa, imependekezwa kuwa suala la mgombea kama yuko peke yake kwenye nafasi husika, asitangazwe kuwa amepita bila kupingwa kama ilivyokuwa zamani. Muswada huo unapendekeza kuwa kama itatokea hivyo, basi apigiwe kura za ndiyo na hapana. Iwapo atapata kura nyingi zinazomkubali, atatangazwa mshindi na kama nyingi zitamkataa hatatangazwa.

Sambamba na hayo, ofisi ya msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ilikuwa ikidaiwa kuhodhi nguvu nyingi, muswada umependekeza mabadiliko kadhaa ambayo yanaipunguzia madaraka hayo ambayo yalionekana kikwazo kwa baadhi ya vyama vya siasa.

Kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma, imependekezwa kuwa maofisa watendaji wakuu wa taasisi hizo, wapatikane kwa ushindani badala ya mfumo wa sasa ambao unaruhusu mamlaka ya juu ya uongozi, yaani Rais kuwateua. Kwa kufanya hivyo, iwapo sheria hiyo itapitishwa, pindi nafasi ya mtendaji mkuu wa taasisi inapokuwa wazi kwa sababu ziwazo zote, watu wataomba na kufanyiwa usaili badala ya kuteuliwa na Rais.

Miswada hiyo imewasilishwa bungeni ikiwa baada ya kumalizika kwa vikao mbalimbali vya mashauriano tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani Machi, 2021. Hayo ni matokeo ya kikosi kazi kiliochoundwa na Rais kupokea maoni na kufanya utafiti wa masuala ya demokrasia na utawala bora pamoja utawala wa sheria nchini.

Aidha, kwa serikali kuwasilisha miswada hiyo, imedhihirika kuwa imesikia kilio cha muda mrefu kuhusu uendeshaji wa masuala ya siasa, ukiwamo upungufu uliokuwa ukilalamikiwa kuhusu muundo wa sasa wa NEC ambayo pamoja na kuonekana kinadharia ni huru, ilikuwa ikidaiwa haina uhuru wowote zaidi ya kuingiliwa na mamlaka za serikali na baadhi ya vyama vya siasa.


Kutokana na kilio hicho ambacho kwa kiasi kikubwa kilitokana na vyama vya siasa, hatimaye serikali imefanyia kazi na kufikia hatua hiyo licha ya kwamba kiu kubwa ya vyama vya siasa ilikuwa katiba mpya kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani mwaka 2025.

Wahenga wanasema ni heri kuwa na kidogo kuliko kutokuwa nacho kabisa. Kiu kubwa ya wadau masuala ya siasa na demokrasia ilikuwa Katiba mpya lakini serikali imeona ianze na mabadiliko ya sheria ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kuwa zinaathiri mfumo wa demokrasia. Kwa kidogo hicho kilichofanywa na serikali, wadau wakubali kuwa kuna hatua imefikiwa kuliko ambavyo serikali ingekaa kimya kabisa.

Katika hili lililofanyika kwa kuwasilishwa miswada ya mabadiliko ya sheria hizo, ni dhahiri kwamba serikali imesikia kilio cha wadau wa siasa na demokrasia vikiwamo vyama vya siasa. Kwa mantiki hiyo, serikali inastahili pongezi na imedhihirisha kwa vitendo kwamba ni serikali sikivu kama ambavyo imekuwa ikijipambanua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Nishati mbadala iwe nafuu watu waachane na mkaa

Na Sabato Kasika

**JANUARI** 31, 2025 itakuwa mwisho wa taasisi kutumia kuni na mkaa ili kulinda mazingira kwa kuepuka ukataji miti ovyo kwa ajili ya nishati hiyo inasemekana inachangia katika uharibifu wa mazingira.

Ni maagizo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo, wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya hatua zinazochukuliwa na serikali kulinda mazingira.

Katika ufafanuzi wake ni kwamba taasisi zote zinazohudumia watu wasiopungua 100, mwisho wao wa kutumia kuni na mkaa ni Januari 31, 2024 na inayohudumia watu kuanzia 200, mwisho ni Januari 31, 2025.

Hatua hiyo ya serikali inakuja ili kulinda mazingira, kwa kuwa hekta 46,960 ambazo ni sawa na asilimia 26 ya ardhi, huharibiwa kila mwaka kutokana na ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.

Niipongeze serikali kwa hatua hiyo ambayo huenda ikapunguza msururu madareva magari pikipiki na baiskeli, ambavyo vimekuwa vikitumika kubeba nishati hiyo kutoka shamba na kwenda kuuza mijini.

Lakini ninadhani kuna haja ya kuuliza je, serikali imejiandaaje kuwasaidia wanaotumia mkaa na kuni majumbani ili waingie katika matumizi ya nishato mbadala kamaa gesi bila usumbufu?

Ninasema hivyo kwa sababu sidhani kama Watanzania wote wanaweza kumudu bei ya mitingi midogo ya gesi ambayo huuzwa kati ya wa Sh 23,000 na Sh. 25,000, hivyo nao wangetazamwa kwa jicho la ziada.

Wakati serikali inajipanga kupiga marufuku matumizi ya kuni na mkaa, kundi hilo ambalo ni kubwa zaidi nalo lingewekewa mazingira ya kupata nishati mbadala kwa gharama nafuu.

Ni kweli mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaendelea kutokea katika maeneo mbalimbali nchini na duniani kote kwa ujumla ni dalili tosha kuwa binadamu wamefanya uharibifu mkubwa wa mazingira yanayowazunguka hasa kwa kukata miti ovyo.

Hivyo kuzuia matumizi ya kuni na mkaa hakuepukiki, lakini njia nzuri ya kuwanusuru watumiaji wa nishati hiyo nayo haiepukiki, kwani sidhani kama wote wanaweza kununua mitingi.

Pamoja na hayo, kukomesha ukataji wa miti holela kunahitaji nguvu ya ziada kutoka kwa wadau wote kuanzia familia, kitongoji, kijiji, mtaa tarafa, wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla.

Jamii yote ikihusika katika vita hii, itakuwa ni rahisi kurekebisha na kurudisha miti inayokatwa, kwa ajili ya uchomaji mkaa na kuni, lakini zaidi sana, nishati mbadala iwe na bei nafuu.

Ni muda mrefu tangu serikali ikemee biashara hiyo, lakini bodaboda, baiskeli na magari vimekuwa vikiingia katika mkoa wa Dar es Salaam, vimekuwa vimesheheni maguni ya mkaa kwa ajili ya biashara.

Hatua hiyo inaonyesha kuwa kuna kundi kubwa linalohudumia familia kupitia biashara ya mkaa, hivyo ni vyema pia waelekezwe mbinu za kujiandaa kufanya biashara mbadala.

Dar es Salaam ni moja ya miji yenye soko kubwa la mkaa ambalo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amewahi kukariri ripoti ya mazingira ya mwaka 2014 kuwa linaongoza kwa matumizi ya nishati ya mkaa.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa Dar es Salaam hutumia tani 500,000 kwa mwaka jambo ambalo linahitaji nishati mbadala, vinginevyo kutatokea madhara makubwa yanayohusisha uharibifu wa mazingira.

Kwa kuwa lengo la serikali kuwa na teknolojia mbadala ambayo itasambazwa kwa wananchi, ili watumiaji wa mkaa wabadilike, wito wangu bado ule ule wa kupunguza gharama.

Hilo lingefaa kwenda sambamba na kuweka mazingira ya kuwawezesha wafanyabiashara ya mkaa na kuni kuwa na shughuli au biashara nyingine ya kufanya ili misitu iweze kuwa salama.

FIKRA MBADALA

# Watanzania tujifunze kuwa na shukrani



Pascal Mayalla

MTU ukiwa na shida fulani kubwa, mfano una dharura unahitaji Sh. milioni moja, ukabisha hodi kwa majirani, ndugu, jamaa na marafiki kuwaomba.

Kila unayemwomba hana kiasi hicho, anakwambia nina Sh. 100,000. Kwa vile shida yako ni Sh. milioni moja, kiasi hicho hakiwezi kusaidia kitu.

Swali linakuja, je, utaacha kuipokea na kuendelea kutafuta Sh. milioni moja au utaipokea na kushukuru kisha utaendelea kutafuta kiasi kilichobaki kufikia lengo lako?

Huu ni wito kwa Watanzania hasa wanasiasa kutoka upinzani, wadau wa demokrasia na wanaharakati. Najua mnataka Katiba mpya, tume huru na shirikishi ya uchaguzi na sheria nzuri ya uchaguzi zenye kutoa haki kwa kila Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa.

Pamoja na hayo, nawasihii pokeeni hiki kidogo mlichopewa. Shukuruni kwa kidogo, kisha endeleeni kutafuta hicho kikubwa. Wahenga wanasema haba na haba hujaza kibaba. Safari ni hatua na huu ni mwanzo.

Pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa mabadiliko ya Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi.

Tanzania, kitu inachohitaji kwanza ni mabadiliko ya katiba ndipo tuje kwenye mabadiliko ya sheria. Madam sasa tumeletewa mabadiliko ya sheria, tuyapokee na tushukuru kisha tuendelee kuomba mabadiliko ya katiba ili yaendane na mabadiliko ya sheria hizi.

Nimeianza makala hii kwa kusisitiza umuhimu wa kuwa na shukrani kwa madogo ili tupatiwe makubwa kwa sababu kilio kikubwa cha demokrasia yetu nchini Tanzania ni Katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika mwaka 2025.

Muda ulibaki kufikia mwaka 2025 ni muda mfupi kwa mchakato wa Katiba mpya, hivyo serikali yetu sikivu ikaona tuanze na mabadiliko ya sheria za uchaguzi na Tume ya Uchaguzi.

Kwa vile tulichokitaka ni kikubwa na tumekikosa, tupokee kwanza hiki kidogo kilichopatikana na kushukuru kwa kusema asante, kisha tuendelee kuomba kile kikubwa tunachokihitaji.

Kwenye safu hii, nimeandika zaidi ya mara 10 kuhusu hitaji la Katiba mpya, mabadiliko ya katiba, sheria ya uchaguzi na mambo ya demokrasia. Miongoni mwa mada hizo ni "Pongezi Rais Samia, Serikali, Kukubali Kubadili Sheria ya Uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi. Tuanze na Katiba Kwanza Ndipo Sheria"; " Fupa hili la katiba, lilowashinda wanaume wanne je, mwanamke mmoja ataliweza?"

Zingine ni "Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani: Je, wajua kuna wanawake wana uwezo mkubwa kuliko wanaume ila wamekuwa wanabaniwa? "Je wajua kuna fupa fulani la dhulma kwa Watanzania, liliwashinda Nyerere, Mwinyi, Mkapa, Kikwete na Magufuli, Je Rais Samia ataliweza ?

Juzi (Novemba 10) ni kama siku ya ukombozi mpya kwenye demokrasia ya taifa letu la Tanzania kuanza kulishughulikia lile fupa la Katiba lilowashinda marais wanaume wanne kwa kipindi cha miaka 40! Rais Samia, ambaye ni rais mwanamke wa kwanza tangu kuasisiwa kwa taifa hili, ameonyesha ushujaa mkubwa ndani ya awamu yake ya uongozi, akiwa ndani ya kipindi cha miaka miwili tu na miezi kadhaa.

Amepeleka miswada mitatu ya ukombozi mpya wa demokrasia ya taifa letu, imetua Bungeni Dodoma.

Miswada hiyo ni ya Mabadiliko ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo japo ni tume huru, haikuwa shirikishi. Sasa tunakwenda kuunda Tume Huru zaidi ya Uchaguzi ambayo itakuwa shirikishi zaidi kuliko tume iliyopo.

Mingine ni wa mabadiliko ya sheria ya uchaguzi, wenye lengo la kurekebisha kasoro mbalimbali kwenye sheria yetu ya uchaguzi na ule wa kurekebisha ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Miswada hiyo tayari imeshasomwa bungeni kwa mara ya kwanza na tayari iko wazi kwenye tovuti ya Bunge.

Hatua ya pili ambayo ipo sasa ni kwa wadau kutoa maoni yao kuhusu miswada hiyo ndani ya miezi mitatu, halafu mkutano wa Bunge utakaoanza Februari, mwakani, itasomwa kwa mara ya pili ikiwa imejumuisha maoni ya wadau, kisha kujadiliwa na wabunge, hatimaye kupitishwa.

Kitendo cha serikali kuwasilisha miswada hiyo ni uthibitisho wa nia njema na dhamira ya dhati ya Rais Samia kuboresha demokrasia nchini. Kwa hilo anastahili pongezi za dhati na kuendelea kuthibitisha wanawake wana uwezo mkubwa kuliko hata wanaume katika baadhi ya maeneo.

Kwa vile tulichotaka sicho tulichopewa, tulitaka kikubwa tumepewa kidogo, tukipokee na tuna miezi mitatu ya kukijadili.

Tuendelee kuomba kile kikubwa. Kama hiki kimekubaliwa, nina imani hata hicho kikubwa atatuletea kwa vile ameonyesha kuwa ni msikivu kwa yale sisi watoto wake tunahitaji.

**Mungu Ibariki Tanzania**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Viongozi punguzeni hadithi, simulizi ondoeni umaskini



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HISTORIA inatwambia vijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) walivyopata kugoma huko nyuma katika miaka ya awali ya 1960, wakipinga kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), huku wakiandamana na kuhanikiza: 'Afadhali wakati wa Mkoloni'!

Naambiwa walifukuzwa na wengine kusimamishwa masomo, huku baadhi wakichezea bakora kwa kutaka kudhalilisha Taifa huru, lililopata uhuru kutokana na mapambano ya mababu zetu na hatimaye kukamilishwa na Mwalimu Julius Nyerere na wenzake.

Sijui kwa nini vijana hao walifanya hivyo lakini pengine walikuwa na sababu za msingi, kwamba wakati huo mambo hayakuwa yakienda sawa kulinganishwa na wakati wa Ukoloni, ingawa naamini enzi za Ukoloni walikuwa bado wadogo.

Kwa kuwa wakubwa waliliona hili kama utovu wa nidhamu kwa wasomi hao wa kwanza nchini, ndio sababu wakaamua kuchukua hatua, ili kuwa funzo kwao lakini onyo kwa wengine, waliokuwa na wazo kama hilo la kushadidia wakoloni.

Inawezekana walikuwa na haki ya kufanya hivyo ila tu katika jamii zetu hizi za Kiafrika, mkubwa hakosolewi na mara zote yuko juu ya mdogo au mnyonge na ndiyo sababu wakachezea kichapo, kwa kuwa tu mkubwa hakutaka kuadhirika.

Si siri kwamba zamani kulikuwa na mambo mazuri yaliyofanywa nchini, tofauti na sasa. Huduma za kijamii zilikuwa bora pia kulingana na wakati huo na zikaja kuborongwa na waliochukua nchi baadaye na sasa kuanza kuzirejesha upya kana kwamba ndipo tumepata uhuru.

Nakumbuka miaka michache baada ya kupata uhuru, kuna mitaa mijini ilikuwa na lami lakini leo haina. Kulikuwa na mabomba yaliyotoa maji kwa kutumbukiza tu sarafu lakini leo watu bado wanapata maji kutoka visimani na kwenye malambo. Uongo?

Nakumbuka pia katika baadhi ya miji, likiwamo Jiji la Dar es Salaam, kulikuwa na mfumo wa majitaka kuchukuliwa majumbani kupitia mabomba maalumu na kumwagwa baharini. Leo hii kila nyumba ina shimo la majitaka ambayo hutapishwa mitaani kila nyakati za mvua!

Zamani umeme ulikuwa wa kumwaga, enzi hizo tukiita stima. Leo hii tunashuhudia kulala giza kama jambo la kawaida na tunashangilia na kukubali simulizi kedekede kutoka kwa wahusika wa nishati hiyo na mwishowe kumwachia Mungu.

Ukithubutu kuuliza, utaambiwa watu wameongezeka na ndiyo sababu ya hali hiyo. Utasikia wakati tunapata uhuru, watu tulikuwa wachache na sasa tumekuwa wengi kuliko uwezo wa kutoa huduma. Kwani watu wakiongezeka si ndiyo nguvukazi nayo huongezeka au?

Ukweli ni kwamba viongozi wetu wanakosa mipango madhubuti ya kusimamia mambo na kuhakikisha matatizo yanamalizika kwa kudumu badala ya kumalizika kwa muda mfupi na kisha kurejea kuumiza wananchi.

Ukitaka kujua hii, fuatilia Bunge, sikiliza maswali yanayoulizwa, sikiliza majibu yanayotolewa, sikiliza mijadala.

Masuala ni yale yale kila mwaka, kila mkutano na kila kikao. Siku zote ni maji, umeme, miundombinu, dawa na kadhalika.

Ni lini nchi hii itafikia mahali tukaacha kujadili maji ya shida, umeme wa shida, madawati ya shida, barabara za shida na mengineyo? Watu wanakutana kila mwaka na kila mara bungeni, kujadili yale yale bila ukomo na kuangalia kwingine.

Tena utasikia, kwamba Singapore ilianza kama sisi na ilipata uhuru si zamani lakini tazameni iliko hivi sasa! Yaani tunajitekenya na kucheka na kufikia hatua ya kujicheka wenyewe. Miaka zaidi ya uhuru tunachimbiwa vyoo na wafadhili!

Barabara na madaraja hata reli karibu zote tunajengewa na wageni, huku tukiwa na vyuo kibao tukisomesha wahandisi wetu, tuna wahandisi wako mitaani wana kampuni na wafanyakazi, lakini hawapewi kazi kwani bila Mchina hakuna kinachowezekana.

Matokeo yake, watu walipewa dhamana wanakwiba mapesa ya umma na kujinufaisha, tukisia wengine wakijinunulia mijengo Ughaibuni na kutanua na familia zao, huku Wabongo wakiishi kwa maisha ya kusawajika.

Mdhibiti Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anatimiza wajibu wake kwa nia njema kabisa, kwa kutuonesha waliko mapanya na mende waharibifu, tunasimama na kupiga makelele kama mbwa anayebwekea lori akidhani atalizuia kupita, lakini ndio kwanza linamtimulia vumbi.

Ukisikiliza kauli za wanasiasa wa nchi hii, unaweza kudhani kesho nchi itageuka mara moja kuwa pepo, unasimuliwa mali zilizopo nchini kwamba zinaweza kutuendeshea nchi bila matatizo, huku vijana wakitiwa nyoyo za kujiajiri kana kwamba wanapewa mitaji.

Na ili kuwanyamazisha, utasikia michezo ya kubahatisha; kamari kila kona, huku wanabeti kule wanachana mikeka, huku wanacheza sijui biko na kule unaambiwa cheza alfu utajirike, kila redio kila televisheni kinachohanikizwa ni kamari tu na vijana wanazidi kubweteka!

Wanasiasa simameni kidete kupambana na matatizo ya wananchi, badala ya kupiga kelele ili mradi mnanufaisha matumbo yenu huku nchi ikienda mrama, tuache kusifiana kuupiga mwingi, wakati wananchi hawana hata pa kulala au pa kula. Mungu aendelee kutulinda!

# RC Mtanda awafunda wastaafu watarajiwa

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, amewakumbusha wastaafu watarajiwa kufanya maandalizi mapema ili kukabiliana na maisha baada ya kumaliza utumishi wa umma.

Mtanda alisema hayo juzi mjini Musoma jana kwenye semina ya walimu na watumishi wa ofisi ya mkuu wa mkoa wanaotarajia kustaafu miaka mitano ijayo.

Katika semina hiyo, alisema zaidi ya wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) 200 na watumishi wa ofisi yake wanatarajiwa kustaafu ndani ya miaka mitano ijayo.

"Ni muhimu kufanya maandalizi mapema, ili baada ya kustaafu maisha yaendelee kama kawaida, hivyo ni vyema mkubaliane na ukweli kwamba mnakwenda kustaafu," alisema Mtanda.

Alisema mtumishi akishakubaliana na ukweli huo, hana budi kujiandaa mapema, kwa kuwa kufanya hivyo atakuwa katika mazingira mazuri muda wa kustaafu utakapofika.

"Semina hii pamoja na mambo mengine inalenga kuwakumbusha na kuwataka walimu na watumishi kuanza maandalizi mapema, ikiwamo kupanga na kuandaa shughuli za kiuchumi mtakazofanya mara baada ya kustaafu," alisema.

Mtanda alisema shughuli zenyewe wanazotakiwa kuzifanya, ni zile ambazo zitawachangamsha na si kushinda nyumbani tu.

Aidha, aliwakumbusha wastaafu hao watarajiwa kuandaa makazi mazuri ambayo yatakuwa karibu na huduma za kijamii, ili wasihangaike kutumia muda mrefu kufuata huduma hizo ambazo zitakuwa zinahitajika mara kwa mara kutokana na umri wao wa uzee.

Akimkaribisha Mkuu wa Mkoa, Katibu wa CWT Mkoa wa Mara, Suzan Shesha, alisema wastaafu hasa walimu, wamekuwa wakijiingiza katika biashara ambazo hawana uzoefu nazo na kujikuta wanamaliza mafao bila kuwa na kitu.

Alifafanua kuwa wastaafu hujiingiza kwenye mikopo yenye masharti magumu ambayo inasababisha wafilisike mapema mara tu baada ya kustaafu.

"Hivyo ninaamini semina hii itatusaidia kujiandaa vyema, kwa ajili ya maisha ya ustaafu tukiwa tunajua ni lipi la kufanya ili kukabiliana na maisha uraiani," alisema Shesha.

Alisema watumishi wanaotambua kuwa kuna maisha baada ya kustaafu, ila bahati mbaya ni kukosa mbinu za kuendesha maisha baada ya utumishi, na kwamba semina hiyo ni muhimu kwao.

# MNEC akemea wana CCM siasa za majitaka

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kupitia Mkoa wa Morogoro, Jonas Nkya, ameyataka makundi ya vijana na wanawake wa chama hicho kuachana na siasa za majitaka.

Amesema makundi hayo yanapaswa kuondokana na fikra kwamba mtu anayetoa misaada anatafuta uongozi na badala yake kuangalia miradi itayowainua kichumi na kuondokana na umaskini.

Nkya alisema hayo juzi wakati akikabidhi msaada wa bajaji yenye thamani ya Sh. milioni tisa kwa muungano wa vikundi 21 vya ujasiriamali katika Bonde la Ruhembe wilayani Kilosa ambavyo vilijiunga kwa ajili ya kufanya shughuli za kujiongezea kipato kwa njia halali.

Alisema wako baadhi ya wanasiasa wanaoona mtu anayetoa misaada lengo lake ni kutaka nafasi fulani kumbe wengine wana lengo la kukisaidia chama kutekeleza ahadi walizoahidi kipindi cha uchaguzi. "Mimi ni Mjumbe wa NEC. Tunafanya hivi kwa ajili ya kurudisha imani kwa wananchi kuendelea kuiamini CCM. Wako watu wanajua tukitoa misaada kama hivi basi tunataka nafasi za udiwani au ubunge. Nikitaka kugombea ninagombea tu bila kutoa msaada," alisema.

Alisema amekuwa akipigwa vita na baadhi ya wanaCCM ambao wanadhani kila anachokifanya kina lengo la kuwania nafasi fulani wakati anafanya hivyo kutokana na nafasi yake ya NEC ambayo anaitumikia kwa sasa.

"Nimekuwa nikitukanwa sana na baadhi ya vikundi vya watu miongoni mwao ni wana CCM wenzangu. Lakini wanajisahau kuwa haya ninayoyafanya watakuja kusimama kwa umma kifua mbele kuelezea pindi kampeni zitakapofika," alisisitiza.

MNEC huyo waliwataka wanakikundi hao kuendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa ameonyesha kuwajali na kusaidia makundi mbalimbali yanayojishughulisha na ujasirimali bila kuangalia itikadi za vyama.

Nkya aliwataka vijana kuacha kusubiri kusemewa na viongozi jinsi Rais Samia anavyotekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, wakati wanajionea kazi kubwa inayofanywa.

Alisema anashangazwa na kundi hilo la vijana wa vyuo vikuu na vya kati kukaa kimya kuelezea mafanikio yaliyopatikana chini ya Rais Samia katika miaka miwili ya uongozi wake kwenye sekta mbalimbali zikiwamo elimu, afya, miundombinu na uendelezaji wa miradi mikubwa mpaka wasemewe na wapinzani.

Awali, Mwenyekiti wa Kata ya Mikumi, Omary Nyarutu, akizungumza kwa niaba ya muungano wa vikundi hivyo, alimshukuru Nkya kwa kuwasaidia bajaji hiyo ambayo itakuwa kama mbegu kwa ajili ya kuzalisha mtaji itakayotumika kama dhamana ya kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kulia), akikabidhi kitambulisho kwa mmoja wa wananchi wakati wa uzinduzi wa utoaji wa vitambulisho vya uraia (NIDA) katika Kijiji cha Lweje, Kata ya Mkoka, wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wahitimu CBE wapewa mbinu za kujiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

KATIBU Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, amewataka wahitimu wa Chuo cha Elimu ya Biashara CBE kutumia elimu waliyoipata kujiajiri na kuajiri wengine badala ya kusubiri kuajiriwa

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 58 ya chuo hicho yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC).

Kwenye mahafali hayo kulikuwa na wahitimu 1,226 wa ngazi mbalimbali wakiwamo wa stashahada, shahada na shahada za umahiri.

Alisema wahitimu hao wanapaswa kutambua umuhimu wa elimu ya ujasiriamali waliyoipata chuoni hapo kwa kuwa itawafundisha namna ya kuwa wabunifu na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi.

Kwa elimu mliyoipata mnatakiwa kwenda kutengeneza ajira kwa wengine badala ya kuwa tegemezi wa kuhangaika kutafuta kuajiriwa nyinyi nendeni mkajiajiri na kuajiri wengine," alisema Dk. Abdallah.

"Ninyi mmepata elimu bora kwa hiyo nendeni mkaitumie kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayosaidia ustawi wa jamii na chuo kimeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha mnapotoka CBE mnakuwa na uwezo wa kujiajiri," alisema.

Alisema utandawazi umesababisha mabadiliko makubwa kwa kasi yanayogusa kila nyanja ya maisha hivyo ni muhimu kutafuta njia ya kukabiliana na mabadiliko hayo kwenye maisha.

Aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa maono mazuri yaliyosababisha kuanzisha programu atamizi ya baishara ambayo inawapa wanafunzi uwezo wa kujifunza usimamizi wa biashara kwa vitendo wanapokuwa shule.

Alisema programu hiyo na ile ya uanagenzi inawawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo wakiwa shule hivyo wanapomaliza masomo hawasumbuki kutafuta ajira.

Dk. Hashil pia aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuanzisha masomo ya shahada ya umahiri katika usimamizi wa biashara (MBA) mtandaoni kwa kuwa inaonyesha ujasiri na uthubutu wa CBE katika kutoa elimu bora na inayokidhi mahitaji ya sasa ya dunia.

"Kuzindua programu hizi kunaweka iwango vipya vya ubora na upatikanaji wa elimu ya juu nawapongea kwa kufungua milango ya fursa kwa wanafunzi na wataalamu ambao wanatafuta kujiendeleza bila kujali umbali," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya sita inathamini na kupongeza mafanikio ya chuo cha CBE na itaendelea kufanyia kazi changamoto ya miundombinu ya vyuo vyote vya elimu ya juu kikiwamo chuo hicho ili kuvuka changamoto hizo.

Alikitaka chuo hicho kuwaendeleza walimu wake na kuwekeza kwenye programu za kisasa za kufundisha, mbinu za kujifunza na mitaala ili kuhakikisha elimu bora inayokidhi viwango vya kimataifa.

"Wekezeni kwenye vifaa vya teknolojia madarasani ili kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia na chuo kifanye tafiti zinazolenga kutatua changamoto zinazoikabili jamii na kutoa rasilimali kwa walimu na wanafunzi kushiriki katika miradi ya utafiti na uvumbuzi," alisema.

Naye Mkuu wa chuo hicho, Profesa Edda Lwoga, alisema wahitimu hao wamehitimu katika masomo mbalimbali yakiwamo ya usimamizi wa biashara, masoko, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na ugavi.

Profesa Lwoga alisema chuo hicho kimejitahidi kwa kiwango kikubwa kuwafundisha wahitimu ili wanapohitimu waweze kujiajiri na kuajiri wengine badala ya kuhangaika kutafuta ajira.

"Tangu mwaka 2022 tulianzisha programu atamizi za biashara ambapo wanafunzi wetu wenye mawazo ya biashara na bunifu mbalimbali wanatuletea mawazo yao tunayalea na wanaweza kuanza kufanyabiashara wakiwa chuoni na tunashirikiana na taasisi mbalimbali.

# MAISHA

NOVEMBA 12, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*



Ukurasa 14

## Saladi ya tango

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Ongeza ubunifu kupangilia nyumba yenye nafasi ndogo






Ukurasa 13




Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | C | H | I | Z | I |
| A | ■ | ■ | ■ | M | ■ | N |
| A | ■ | A | R | A | ■ | G |
| H | A | O | ■ | R | A | I |
| I | ■ | M | I | A | ■ | Z |
| R | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| A | P | E | T | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MIA, NIA, OTA, KUU, MWAKA, MANDE, ELEWA, SIMBA, KIBONDE, AMBULIA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA

MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unajua kuna uchawi ulevi wa pombe?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuangalia duru la ulevi na hasa kwa vijana. Makala mbili zilizotangulia tumeangalia mambo mengi, ikiwa ni pamoja na madhara ya unywaji wa pombe kupita kiasi.

Leo tumulike zaidi vyanzo vya ulevi wa aina hiyo. Kwa nini mtu anywe pombe hata kumpotezea mwelekeo wa maisha. Nilisema wiki iliyopita kuwa asili ya mtu pia imechangia sana tabia hiyo.

Yuko anayelewa sana leo, kumbe ulevi ni chapa kwenye familia tangu enzi za mababu zake. Hii ni roho kubwa inayoangamiza watu wengi.

Roho ya ulevi ni silaha inayotumiwa na ibilisi pamoja na mawakala wake kuangamiza na kupoteza hatima za watu wengi. Utajiuliza, inakuwaje hapo?

Ukiacha chanzo cha asili ya mtu, uko uchawi wa ulevi wa pombe, bangi, sigara na kadhalika ambao unaweza kutupwa juu ya mtu na kumfanya asiwe na akili timamu.

Unaweza kumwona mtu uliyekuwa unamfahamu, mtaratibu, mchakarikaji kutafuta fedha lakini ghafla anakuwa mlevi wa ajabu. Watu wanaanza kumshangaa. Kumbe chanzo kingine ukiacha asili ya mtu ni pale anapowekewa uchawi kwenye pombe na kumfanya kushindwa kuacha unywaji huo wa kupindukia.

Kuna roho za ulevi wa kurithi, hasa wa pombe. Roho hizi hutokana na maagano yaliyowekwa na mababu kwenye koo. Madhara ya ulevi ni makubwa sana. Wengi wamepoteza mwelekeo wa maisha.

Ndoa nyingi na familia nyingi zimesambaratika kwa sababu ya roho ya ulevi. Ni roho inayopaswa kushughulikiwa kwa nguvu zote ili kuokoa jamii yetu kwa kuwa inashambulia sana hasa vijana.

Roho hii ya ulevi imevuruga wengi kwa kuwa imechipua roho nyingine iitwayo roho ya umaskini. Hii ni ngome kubwa duniani iliyoshikilia watu na kuwafanya waishi katika mateso makubwa. Imefanya wengi washindwe kufurahia uwepo wao duniani.

Mtu atauliza, umaskini ni nini? Umaskini ni kuwa na mzunguko wa madeni. Ni kuwa na mapato yasiyokidhi mahitaji. Mtu anakuwa na matumizi makubwa kuliko kipato chake.

Umaskini ni kutokuwa na uwezo wa kumiliki kitu chochote katika maisha, iwe ni nyumba, gari, shamba, ardhi na kadhalika. Ni kuishi kwa kusaidiwa na watu. Hapa mtu anakuwa hana uwezo wa kujisimamia, anaishi kwa kuomba omba.

Umaskini ni roho mbaya sana imefanya watu wengi waishi kwa kudharauliwa. Umaskini umeangamiza vijana, wazee, watoto, wanawake na wanaume. Vijana wengi wamejikuta wakijiingiza katika makundi mabaya kama ujambazi ili tu wapate chakula.

Mpenzi msomaji, hapo juu nimejaribu kuzioanisha roho mbili, ya ulevi na ya jinsi zinavyoambatana kuharibu hatima ya mtu. Ziko ndoa zimesambaratika kutokana na ama baba au mama kuwa mlevi kwenye familia.

Na ulevi huu ni ule unaosababisha ugomvi usioisha ndani ya nyumba kiasi cha amani kutoweka. Ukienda kwenye mahakama zetu za mwanzo, utakutana ma mashauri mengi yanayohusu madai ya talaka.

Ni ndoa zilizoanza vizuri, maisha yakaendelea hadi Mungu kuwajalia watoto kadhaa. Ni ndoa zilizokuwa na uchumi mdogo wakati zinaanza na zilivyoendelea uchumi ukaongezeka, wengine wakanunua gari, wengine wakajenga nyumba.

> **"Ndoa nyingi na familia nyingi zimesambaratika kwa sababu ya roho ya ulevi. Ni roho inayopaswa kushughulikiwa kwa nguvu zote ili kuokoa jamii yetu kwa kuwa inashambulia sana hasa vijana.**

Wakati sasa wanapotaka kuanza kuyafaidi matunda ya jasho lao, ndipo ibilisi wa pombe anapowavamia kuvuruga mafanikio yao. Siku zote shetani hashughulikia na mwanzo bali husababisha mtikisiko katikati na mwishoni.

Hapo ndipo baadhi ya watu wenye familia zao nzuri huanza kubadili mwelekeo. Anaweza kulogewa roho ya ulevi au chanzo cha asili yake kinaweza kumfuatilia.

Baba sasa ana gari, anaanza kutoa lifti kazini. Pia kutafuta mchepuko wa kustarehe, anasahau kabisa maisha kabla ya neema aliyonayo. Anarudi nyumbani muda mbaya, amelewa, akiulizwa mkali na wakati mwingine mama anaambulia kichapo.

Iko familia moja naikumbuka pale Mbezi Mwisho. Mwanamume alikuwa mlevi wa kupindukia. Siku moja mkewe akampa hela kununua nyama. Muda ukaenda sana jamaa harudi. Jirani ilikuwapo baa kubwa ya pombe.

Mama kumfuatilia kwani bucha ilikuwa jirani tu, akamwona mumewe juu ya stuli ndefu baa, yuko chakari. Akamwuliza nyama iko wapi, akawa anacheka.

Kumpekuwa mfukoni, amebakiza Sh. 3,000. Akazichukua naye akaagizia bia na kumwambia, "ngoja tulewe hakuna kupika tena".

***Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki ijayo tutaona ulevi ulivyokithiri kwa vijana na maoni yao. Una maoni? Ujumbe 0715268581***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Uwezo wa kutafsiri, kupima unakutambulisha ulivyo

MTU mzima akikosea huchutama, akihisi kuna mahali alijisahau na alinyanyua mabega mbele ya waliomwamini na kumwona mtu anayeweza kuwavusha kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Lakini kiburi huponza wengi na kujikuta wakipoteza au kupotea katika nafasi fulani.

Majuzi, kuliibuka mjadala mzito kwenye mitandao ya kijamii na ndani ya Bunge baada ya kusambaa video moja ikiwaonyesha wanafunzi na msanii wa kizazi kipya, wakiserebuka wimbo wenye shangwe la kutosha wa 'honey'.

Kwa asiyeujua hawezi kuona ni namna gani huwa unawafanya watu kujizima data kichwani na kunengua kwa kukata mauno balaa.

Kitendo hicho kikatafsiriwa vibaya kama si cha kiungwana kwa wanafunzi hao. Eti wimbo huo una kasoro za kimaadili kutokana na maudhui yake kukinzana na maadili ya Mtanzania!

Huo wimbo umepata baraka zote za Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Wameona maudhui yake hayakiuki kanuni, taratibu za sanaa na unakidhi matakwa ya sheria kama alivyoona mdhibiti mkuu wa kazi za sanaa nchini.

Kama tunataka kupambana na mmomonyoko wa maadili, mamlaka za serikali za nchi yetu, zishughulikie mzizi wa tatizo na si matawi.

Kama wimbo wa msanii huyo hauna maudhui mazuri, kwa nini mamlaka ziliruhusu usambae? Kuna nyimbo ngapi za muundo huo zimeachwa zinapigwa maeneo mbalimbali?

Je, tunamlindaje mtoto wa Kitanzania kusikiliza au kutazama hizi nyimbo akiwa shuleni? Tumejiuliza anapokuwa nyumbani, mtaani, kwenye harusi na sherehe nyingine za kijamii, inapopigwa hiyo nyimbo huwa hawachezi?

Je, hao walimu waliokutana na adhabu batili ya kiongozi wa kisiasa, hana hisia ya kupenda kuburudika kwa nyimbo kama hizi?

Kuagiza walimu wavuliwe vyeo vya ukuu wa shule, kisa wameruhusu kuchezwa wimbo huo ni kutowatendea haki na ni kushughulika na matawi, badala ya shina.

Hivi kuna siku mliwahi kukemea au kutangaza marufuku ya wasanii kutotumia nguo za shule za msingi na sekondari kunengua na kukata mauno jukwaani?

Suala hapa, sasa serikali ijipange kulinda hiki kizazi, sio shuleni. Kwa hiki kilichotokea, sasa huko shuleni zitaimbwa kwaya na na kaswida. Swali la kujiuliza, Je, huko mtaani tatizo litakuwa limekwisha?

Kabla ya kuagiza kuvuliwa vyeo walimu hao, walipaswa kusikiliza, kupewa onyo au karipio, kama hatua muhimu za kinidhamu. Ila hili la kukurupuka tu na kusema achia madaraka, simama na kazi! heee hapana!

Wewe unaridhika elimu nchini mwetu iendeshwe hivi?

Tunashukuru Bunge letu limeguswa na tatizo hili. Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na wabunge kwa kuliona tatizi na kupingana na uamuzi uliochukuliwa kushughulikia tatizo.

Ashukuriwe Mungu, tayari walimu wakuu wawili wa shule za msingi Mlimani na Tunduma TC, waliovuliwa vyeo vyao na kusimamishwa kazi kisa video ya 'Honey' wamerejeshwa kazini.

Hiyo ni baada ya hoja kuibuka bungeni na Spika, Dk.Tulia Ackson, kuagiza walimu hao kurudishwa kazini na kupewa nafasi ya kusikilizwa.

Siku moja baadaye, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) likamnukuu Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tunduma, Seleman Kateti, akisema kutokana na kauli ya Spika, wao kama halmashauri wamelazimika kuwarudisha kazini wakuu hao wa shule kwa sababu taratibu hazikufuatwa.

Agosti 8, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani mkoa wa Njombe, alionya wateule wake kuacha kuinua mabega, badala yake wahudumie wananchi kulingana na viapo vyao.

Najiuliza kama ndivyo! wakubwa huko wizarani, serikalini, hawakumbuki onyo la Rais Samia akiwa Njombe?

Msinihukumu kwa hili ninalowakumbusha nalo kuhusu onyo la Rais Samia. Nawakumbusha kwamba uwezo wa kutafsiri, kupima unakutambulisha jinsi ulivyo! Hebu tutoke huko bwana, tufanye kazi tuliyotumwa!

***•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***



ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA HAJI BAKARI NA BI SAUMU SHABAN BAADA YA KUFUNGA NDOA NOVEMBA 4, MWAKA HUU KATIKA KIJIJI CHA HACHWI, WILAYA YA KONDOA MKOANI DODOMA.







## MITINDO









# UMEALIKWA CHAKULA CHA JIONI?

Je, kuna kitu kizuri zaidi kuliko kwenda nje kwa ajili ya kupata chakula cha jioni au kufurahia usiku na marafiki zako?

Hakika ni jambo la kupendeza na linafurahisha kama ukiwa katika maeneo hayo na mwenye kujiamini zaidi.

Kuna mapendekezo mawili ambayo yanasimama juu ya kuweka mwonekano mzuri.

Kwa upande mmoja, kuchanganya vazi la leggings na juu kuvaa koti la wazi na kukamilisha kwa viatu vya mchuchumio au visigino virefu.

Kwa upande mwingine, kuna wazo la kuchagua la kuvaa shati la mikono mirefu na suluari au sketi ya hariri au velvet.

Unaweza kuchanganya kwa kuvaa na sweta au koti la blazi.

Katika mazingira hayo mavazi yenye mvuto kama hayo ni jambo la kuzingatia zaidi.

Wakati wa kuchagua aina hizi za nguo ni muhimu kuangalia ukubwa wa kiuno kama inakutosha na ubora unaokubalika.

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# MWANAMKE USAFI

UREMBO si uzuri wa sura ila ni namna unavyoweza kujiweka maridadi kwa kuhakikisha usafi wa mwili na mavazi.

Leo katika safu hii, nitakuelekeza maeneo ya muhimu kwenye mwili wa binadamu unatakiwa ufanyiwe usafi vizuri.

**SIKIO**

Nyuma ya sikio na kwenye kona kona za sikio kuna weusi fulani hivi unaoonyesha sikio halisafishwi.

Unatakiwa kuhakikisha unatumia dodoki kusafisha sikio lako kwa maji na sabuni pindi unapooga.

**KITOVU**

Kama hauzingatii usafi, utakuta kitovu kina magamba meusi kiasi kwamba kunabadilika hadi rangi.

Ikiwezekana mara moja kwa mwezi chukua kitambaa chovya kwenye maji ya uvugu uvugu safisha kitovu chako taratibu.

**USAFI WA MIGUU**

Unamkuta mdada ana dhahabu mbili tatu hapa na pale kajisugua mwili katakata. Lakini mguu ana zagamba.

Sio lazima ukaanike miguu uoshwe na watu saluni, hata kwako unasafisha miguu yako na inang'aa tu, unahitaji beseni, maji ya uvuguvugu, shower gel, brashi na ubao wa kusugulia gaga unaopatikana maduka ya urembo kwa 1,500.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**



# Saladi ya tango, mayai ya kuchemsha

SALADI ya tango na mayai ya kuchemsha unaweza kuiandaa nyumbani kwako ndani ya dakika 10 pekee na ukafurahia mlo wako.

**Mahitaji**

Chemsha mayai yako matatu, safisha matango mawili, mbaazi za kijani, kabeji, mayonise kwa ajili ya kuongeza ladha, sosi cream, chumvi na pilipili.

Namna ya kuandaa

Jinsi ya kuandaa saladi ya mayai ya kuchesha ni rahisi na unaweza kuandaa kwa muda mfupi na ukafurahia mlo wako.

Kata tango vipande vipande katakata mayai na kabeji.

Weka mchanganyiko wako kwenye bakuli, ongezea mbaazi za kijani, chumvi, pilipili, mayonnaise na sour cream. Changanya viungo vyote.

Tayari saladi inaweza kutumika mara kwa aina yoyote ya chakula unachopendelea kwa wakati huo.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# ONGEZA UBUNIFU KUPANGILIA NYUMBA YENYE NAFASI NDOGO

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini wanaishi katika nyumba za kupanga. Kutokana na hali halisi ya familia za Kiafrika, ni chache ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba nzima au kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo za Kiafrika, nyingi huwa zinajumuisha zile kama zinavyojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended family', hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo, ili umudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia iliyopo, lazima ubunifu na akili nyingi itumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa samani katika nyumba hiyo ndogo ni lazima uhakikishe zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni, unaweza kuweka ambayo inakuwa



na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu na vinginevyo.

Pia unaweza kutumia sehemu ya ukuta 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine ikiwamo vyombo hasa jikoni.

Na ili ufanikishe kwa vitu vichache unavyokuwa umepanga kuweka kwenye nyumba hiyo ndogo ni vizuri kupima kwanza ukubwa wa eneo lako kabla ya kutengeneza samani zako.

Epuka kuweka vitu ovyo bila kufanya tathmini ya uhakika na ikiwezekana orodhesha idadi ya vitu na vya aina gani vinavyotakiwa kuingia kwenye nyumba hiyo na ambavyo havichukui nafasi kubwa.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fenicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa.

Jambo kubwa la kuzingatia katika kupangilia vitu kwenye nyumba yako ndogo ni ubunifu na kuepuka vitu ambavyo havina ulazima.

Usiweke kitu ilimradi umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingia umuhimu wake na nafasi uliyonayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa samani za ndani, zipo hata ambazo unaweza kuzikunja na kama ukifanikiwa kupata za namna hiyo inakuwa bora zaidi katika kuhifadhi nafasi.

Kwamba unazitumia pale unapoona inahitajika tu, na unaweza kuamua kuzikunjua nyakati za mchana halafu usiku ukakunja.

## Usipitwe vitu muhimu wakati wa sikukuu

**Na Restuta James**

SHAMRASHAMRA za mwisho wa mwaka zimeanza na kama tunavyofahamu huwa zinakuja na gharama zake hasa kwenye mapambo ya sikukuu ya Krismasi ambayo inaambatana na likizo ndefu na fupi za kikazi pamoja na za wanafunzi.

Leo ninakuletea makala kukukumbusha mambo kadhaa yanayoambatana na sikukuu za mwisho wa mwaka za Krismasi na mwaka mpya.

Kwa waliopo mijini, maduka makubwa yaani shopping malls pamoja sehemu za starehe zimeshapamba maeneo yao kwa mapambo ya Krismasi.

Mitandaoni na kwenye majukwaa ya kidijitali, hali ni hiyo hiyo na vingi vinavyokatiza (pop up), kwenye matangazo ni pamoja na mapambo na maandalizi ya sikukuu hizi.

Yapo pia maduka ambayo yametangaza punguzo la bei za bidhaa zake zikiwamo samani za ndani, vyombo, mavazi na huduma kadhaa wa kadha.

Nikukumbushe tu kwamba kama unataka kupamba nyumba yako kwa miti ya Krismasi na mapambo yake, usiache kupitia kwenye mitandao na majukwaa ya kidijitali kujifunza mbinu mpya za upambaji.

Kwenye majukwaa utaona ubunifu wa kupamba mti wa Krismasi, vyumba, milango mikubwa ya nje, bustani na hata ngazi kwa wale wenye nyumba za ghorofa.

Baada ya msomaji mmoja kuniomba nimpe tips za upambaji kwa mwisho huu wa mwaka, nililazimika kutembelea majukwaa mbalimbali ambako nilibaini kwamba wako watu ambayo wamebadili kabisa mwonekano wa sehemu ya nyumba na hasa vibaraza kwa kubandika 'wallpaper' zinazoakisi shamrashamra hizo. Wengine wamenakshi vyumba hasa vya watoto kutokana na watengenezaji wa mapambo hayo kuzalisha yale yanayotawaliwa na rangi za pinki, njano na bluu zilizopoa, ambazo zinajulikana kama rangi za watoto.

Si hivyo tu bali kwa wale watakaohitaji kununua mavazi ya familia, yapo yanayoashiria sikukuu hizo ambayo yanaweza kuvaliwa na familia nzima hasa pajama.

Inashauriwa kuwa kwa kuwa hiki ni kipindi kinachoamsha hisia kwa wengi, ni vyema kutenga muda wa kukaa na familia na ikiwezekana kutembelea eneo mahsusi kwa ajili ya kuimarisha mahusiano.



# Ukosefu wa mbolea sasa kuwa historia

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

UPUNGUFU wa mbolea mkoani Ruvuma na nchi nzima kwa ujumla, utabaki historia baada ya Kampuni ya mbolea ya ITRACOM kuzalisha mbolea inayokidhi mahitaji ya wakulima kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa ITRACOM, Dk. Keneth Masuki. Alisema hayo juzi wakati anazungumza kwenye hafla ya ufunguzi wa ghala la mbolea la kiwanda hicho, Msamala, Manispaa ya Songea.

Dk. Masuki alisema kampuni hiyo imejenga kiwanda mkoani Dodoma ambacho kina uwezo wa kuzalisha mbolea na virekebishi vya udongo zaidi ya tani milioni 1.5 kwa mwaka, hivyo kukidhi mahitaji ya mbolea katika nchi nzima ambayo ni tani 600,000 hadi 700,000 kwa mwaka.

"Uwekezaji wa kiwanda hiki ni wa kimkakati kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa Makamu wa Rais, ndiye aliyeanza hizi harakati za uwekezaji wa kiwanda. Mchakato ulianza mwaka 2020, hivyo uwekezaji ni mkubwa kwa kuwa kiwanda ni kikubwa ambacho kinailetea heshima Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa katika Afrika, hakuna kiwanda kikubwa cha mbolea kama hicho ambacho kinatengeneza mbolea iliyochanganywa mbolea za chumvi chumvi na samadi. Alisema kiwanda kimetokana na mwekezaji ambaye alikuwa na kiwanda kama hicho nchini Burundi.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, ambaye aliwakilishwa na Kapenjama Ndile, alisema matokeo ya kiwanda hicho ni jitihada za Rais Samia ambaye alifanya juhudi za kumshawishi mwekezaji kuhakikisha kiwanda hicho kinaanzishwa nchini kukidhi mahitaji ya wakulima.

Alisisitiza kuwa kufunguliwa kwa ghala hilo mjini Songea ni fursa ya kufungua maghala mengine mengi ya mbolea maeneo ya vijijini waliko wakulima wengi.

"Nimeambiwa ITRAFOM inatengeneza aina tatu za mbolea ambazo ni mbolea ya kupandia (FOMI PANDIA), mbolea za kukuzia (FOMI KUZIA) na mbolea za kuzalisha (FOMI NENEPESHA). Ni matumaini yangu kuwa wakulima watajengewa uwezo kuhusu namna ya kutumia mbolea hizi ili uzalishaji uwe na tija," alisema.

Alibainisha kuwa katika msimu wa mwaka 2022/23 wakulima mkoani Ruvuma walizalisha tani 1,870,800 ya mazao ya chakula, biashara na mboga, sawa na asilimia 95 ya lengo la mavuno ya tani 1.965,072. Kati ya hizo, alisema mazao ya chakula pekee, zilivunwa tani 1,598,163 huku ya biashara zikiwa tani 94,741.




Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (kushoto), akiangalia kazi za mikono zinazofanywa na Umoja wa Wanawake Wachimbaji Tanzania (TAWOMA) wakati akizindua Jukwaa la Uzinduaji kwa mwaka 2023, lililoandaliwa na Asasi ya Kiraia ya HakiRasilimali, juzi jijini Dodoma. **PICHA: WIZARA YA MADINI**

# Serikali yasikia kilio cha wananchi waishio vijiji mipakani mwa hifadhi

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imesema imesikia kilio cha wananchi wa vijiji vilivyopakana na hifadhi za taifa, kwamba itakuja na mkakati wa kutatua migogoro na vikwazo inayojitokeza kati yao na mamlaka za hifadhi za taifa.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo alisema hayo juzi bungeni wakati akijibu hoja za wabunge waliochangia Mpango wa Taifa wa Mwaka 2024/25

Prof. Mkumbo alisema Rais Samia Suluhu Hassan anathamini maendeleo ya watu kuliko kitu chochote na ndiyo sababu amewaagiza (mawaziri) kwenda kuwatumikia Watanzania na siyo kuwaumiza.

"Tumewasikia wananchi wote wanaoishi kando ya hifadhi za taifa. Rais Samia ni muungwana, mpenda haki, mwadilifu na mzalendo kwa taifa lake na Watanzania. Maelekezo yake siku zote ni kuwatumikia Watanzania na siyo kuwaumiza," alisema.

Hata hivyo, alitoa angalizo kwa Watanzania wanaoishi pembezoni mwa hifadhi za taifa kwamba wafuate sheria zilizotungwa na endapo kutakuwa na tatizo au kasoro katika sheria hizo ziletwe bungeni ili zifanyiwe marekebisho.

Kuhusu maoni ya serikali kuzingatia maendeleo vijijini, Prof. Mkumbo alisema serikali imekua ikifanya jitihada za kuhakikisha maendeleo yanapatikana.

Alisema kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imefanikiwa kujenga mitandao ya barabara mbalimbali vijijini.

Prof. Mkumbo pia alisema kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) serikali pia imefanikiwa kupeleka umeme katika vijiji zaidi ya 9,000, kadhalika alisema serikali kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imepeleka huduma ya maji vijijini.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwaagiza watendaji wa serikali kuhakikisha wanachukua hatua dhidi ya watumishi ambao watabainika kuhusika katika ubadhirifu wa fedha katika miradi ya maendeleo.

"Hakuna haja ya kusubiri viongozi waje wilayani kuchukua hatua dhidi ya watumishi waliohusika na ubadhirifu wakati hapo wilayani kuna Mkuu wa Wilaya, Kamanda wa TAKUKURU, Mkuu wa Polisi Wilaya, Mahakama na Magereza".

Kuhusu ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi, Waziri Mwigulu alisema maeneo yote ambayo hayana migogoro serikali itaendelea kulipa fidia.

Alisema maeneo ya wananchi ambayo serikali imeyachukua kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiserikali wananchi husika watalipwa fidia.

# Wananchi wapatiwa elimu kuhusu viwango

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WANANCHI 6,220 katika halmashauri za wilaya za Masasi, Nanyumbu, Newala, Tandahimba na Manispaa ya Mtwara Mikindani, mkoani Mtwara, wamepatiwa elimu kuhusu masuala ya viwango na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Elimu hiyo walipatiwa kuanzia Oktoba 16 hadi Novemva 3, mwaka huu, ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya shirika hilo inayolenga kuongeza uelewa wa masuala ya viwango hapa nchi.

Akizungumza wakati wa kampeni hiyo, Ofisa Masoko TBS, Mussa Luhombero, alisema lengo la shirika hilo ni kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kusoma taarifa zilizopo katika bidhaa, kununua bidhaa zilizothibitishwa ubora wake.

Luhombero alsiema shirika linalenga kuwahamasisha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Alisema kampeni hiyo ya elimu kwa umma imefanyika katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu ikiwemo ya sokoni, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi. Kwa mujibu wa Luhombero, wananchi walijitokeza kwa wingi kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yanayohusu ubora wa bidhaa.

Naye Ofisa Usalama wa Chakula Mwandamizi wa TBS, Barnabas Paul, alisisitiza wajasiriamali na wafanyabiashara kuuza bidhaa zilizothibitishwa ubora na TBS na wenye majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi kuyasajili ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

Paul aliwafafanulia wananchi umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku ikiwa ni pamoja na kulinda usalama na afya ya mtumiaji bidhaa husika na kwa wazalishaji viwango vinawahakikishia masoko ya uhakika na kufanya bidhaa husika kuhimili ushindani kwenye soko.

Aliwataka wazalishaji na wananchi kwa ujumla na kuhakikisha wanakuwa mabalozi wa kuhamasisha ubora katika jamii wanazoishi sambamba na kutoa taarifa katika ofisi ya TBS zilizopo karibu nao.

Aliwataka kupiga katika siku kituo cha huduma kupitia mawasiliano yaliyotolewa iwapo watakutana na changamoto zinazohusu masuala ya ubora wa bidhaa wakati wa manunuzi. Mmoja wa wananchi hao, Halima Abdallah, alisema kabla ya elimu hiyo alipokuwa akienda kununua bidhaa kigezo alichokuwa akikitumia ni kuangalia unafuu wa bei badala ya kuangalia kama imethibitishwa ubora wake.

Miongoni mwa wananchi waliopatiwa elimu hiyo, 158 ni wajasiriamali wanaozalisha bidhaa mbalimbali.

# DUNIA NZIMA YAPATA HOFU

## -Hospitali kubwa zaanza kushambuliwa
## -Wazee, wagonjwa, watoto hatarini Gaza



Baadhi ya raia wa Kipalestina wakikimbia mapigano Gaza Kaskazini.

DUNIA imeanza kuwa na hofu baada Jeshi la Israel kuanza kushambulia hospitali kubwa ambazo zimehifadhi idadi kubwa ya watu.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, tayari ameitaka Israel kukomesha mauaji ya watoto wachanga na wanawake katika Ukanda wa Gaza.

Katika mahojiano ya kipekee katika Ikulu ya Élysée, alisema hakuna uhalali wa shambulio hilo, akisema kusitishwa kwa mapigano kutanufaisha Israel.

Alisema Israel ina haki ya kujilinda, lakini aliomba wasitishe mashambulizi hayo.

Alisisitiza kwamba Ufaransa inalaani vitendo vya kigaidi vya Hamas.

Kiongozi huyo alisema ana matumaini Marekani na Uingereza watajiunga kutoa wito huo.

**HOFU AL-SHIFA**

Hadi jana usiku hali ya wasiwasi imetanda katika hospitali kubwa ya nne katika mji wa Gaza, wakati wanajeshi wa Israel wakiikaribia.

Watu waliokuwa ndani walisema wanasikia milipuko na milio ya risasi karibu na hospitali na kwamba mizinga ya Israel ilikuwa umbali wa mita 100 kutoka jengo hilo.

Mtangazaji wa BBC, Rushdi Abualouf alifanikiwa kuzungumza na mkurugenzi wa hospitali hiyo, ambaye alisema watu 15,000 wapo ndani ya jengo hilo.

Wengi wa watu waliokuwamo ndani ni wazee na wagonjwa, ambao hawawezi kusafari kuelekea kusini ambako Israel imewataka watu kuhamia.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, alisema wamezidiwa na idadi ya watu waliojeruhiwa na wanalazimika kuwatibu watu wakiwa sakafuni.

Wakati huo huo, mapigano katika Hospitali ya Al-Quds yameongezeka usiku wa kuamkia jana.

Inaelezwa meli ya jeshi la wanamaji na vifaru vya Israel vilihusika na shambulizi hilo.

Aidha Mhariri wa BBC wa kimataifa Jeremy Bowen ambaye yuko Israel, alipokea ujumbe wa sauti kutoka kwa daktari wa upasuaji Marwan Abu Saada, ndani ya hospitali ya Al-Shifa akisema wanashambuliwa.

Saada alinukuliwa akisema kuwa chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) kimeshambuliwa, huku sauti za risasi na mabomu zinasikika kila sekunde.

Anasema hakuna mtu anayeweza kutoka hospitalini, na hakuna mtu anayeweza kuingia.

Daktari huyo anaongeza kwamba hakuna maji, chakula wala umeme katika hospitali hiyo.

Wagonjwa wawili ambao walikuwa kwenye mashine za kupumua wamefariki, mmoja wao akiwa mtoto.

Wizara ya afya inayoendeshwa na Hamas pia imeripoti kifo cha mtoto mchanga.

Watu wamepigwa risasi

Saada alisema watu waliojaribu kutoka hospitalini majira ya asubuhi kwa ajili ya kwenda sehemu nyingine salama walipigwa risasi.

Alisema timu ya wahandisi ilikwenda kuangalia jenereta zinazotumika ICU na kitengo cha watoto wachanga, nao walipigwa risasi na mmoja wao amepooza mwili.

Dk. Mohammad Abu Mughaiseb, alisema ikiwa hakuna usitishaji vita au upatikanaji wa msaada wa matibabu, wagonjwa wote waliobakia katika hospitali hizo watafariki na majengo hayo yatageuka kuwa makaburi.

Alikiambia kipindi cha Wikiendi cha BBC World Service kwamba kitengo cha wagonjwa mahututi cha hospitali kuu ya watoto huko Gaza kilipigwa kwa bomu na kuwalazimu timu za MSF na wafanyikazi wengine wa matibabu kushindwa kufanya kazi.

"Timu ya matibabu iliondoka hospitali ya watoto kulikuwa na watoto watano katika chumba cha wagonjwa mahututi. Watoto hawa sasa wameachwa peke yao katika hospitali iliyolipuliwa, hawa watafariki." Alisisitiza.

Dk. Abu Mughaiseb pia alisema uhaba wa dawa ni mbaya kiasi kwamba upasuaji unafanywa bila ganzi.

**QATAR NA MISRI WATOA WITO**

Viongozi wa nchi za Qatar na Misri wamefanya mazungumzo, na kutoa wito wa kupunguzwa kwa machafuko katika Ukanda wa Gaza.

Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sissi alijadiliana na kiongozi wa Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad al Thani kuhusu juhudi za kuhakikisha mapigano yanasitishwa na hatua za kuongeza misaada ya kiutu kwa Wapalestina.

Wawili hao aidha walizungumzia kuongezeka kwa mashambulizi ya Israel na changamoto ya kikanda iliyoko mbele yao inayoupeleka mwelekeo wa hatari.

Naye Mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed Bin Salman ametoa wito wa kumalizwa vita katika Ukanda wa Gaza.

Akiweka msimamo wake na viongozi wa Afrika wanaohudhuria mkutano wa kilele wa maendeleo kati ya Saudi Arabia na Afrika, Bin Salman alisema wanalaani kile kinachotokea Gaza, na hasa mashambulizi yanayowalenga raia na ukiukwaji wa sheria ya kimataifa unaofanywa na mamlaka za Israel.

Mwanamfalme huyo ni mara yake ya kwanza kuzungumzia mzozo huo hadharani tangu ulipozuka mwezi uliopita.

Azimio la pamoja na viongozi kwenye mkutano huo wa kilele limeelezea wasiwasi mkubwa kuhusiana na hali ya kiutu huko Gaza na kutoa wito wa kumalizwa operesheni ya kijeshi na raia kulindwa.

**OMBI LA MPAKA**

Umoja wa Mataifa imeomba Israel kufungua kituo cha mpaka wake wa Kerem Shalom ili misaada zaidi ya kiutu iweze kupita na kuingia Gaza.

Kituo hicho kati ya Gaza na Israel kina uwezo wa kupitisha malori, tofauti na kivuko cha Rafah kinachotokea Misri, ambacho kilijengwa kwa ajili ya watembea kwa miguu.

**NETANYAU AJIBU**

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amemjibu Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kwa kueleza mataifa ya nje yatakiwa kuilaani Hamas na sio nchi yake.

Katika taarifa yake, Netanyahu alisema jeshi lake linajaribu kuwaondoa raia katika mzozo huo, lakini Hamas wanawatumia kama ngao.

Ameonya katika taarifa hiyo kwamba uhalifu unaofanywa na Hamas na ISIS huko Gaza utafanyika tena kesho huko Paris, New York, na duniani kote.

**MAANDAMANO UINGEREZA**

Polisi wa mji wa London walisema wanatarajia kufanyika mandamano makubwa ya kuwaunga mkono Wapalestina na hivyo kuongeza askari wa kulinda usalama.

Maandamano hayo yanaambatana na Siku ya Armistice, ambayo itashuhudia matukio ya ukumbusho yakifanyika katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Eneo lililotengwa zaidi ni Cenotaph na Whitehall, ambalo mamlaka ya jiji ilisema itapiga marufuku waandamanaji wanaounga mkono Palestina kuingia maeneo hayo.

Waziri Mkuu, Rishi Sunak, ameyataja maandamano hayo sawa na ukosefu wa heshimu na kuwataka waandamanaji kutilia maanani hofu na dhiki katika jamii za Wayahudi na Waislamu.



Hospitali ya Al-Shifa.

SAFU

## MAKALA

# NHIF WAPENI UHURU WATUMISHI



Na Magabilo Masambu

**Nafahamu kuna hoja kwamba masuala ya bima ukichangia si lazima unufaike wewe na kwamba unachangia wasiojiweza. Hivi inaingia akilini kwamba wasiojiweza wako ndani mwako lakini sheria haiwahusu?**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya ni mpango wa bima ya afya wa kisheria ulioanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 8 ya mwaka 1999 ili kuwezesha upataji wa huduma za afya kwa wanachama wakuu na wategemezi wao.

Uanachama huo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya Sura Na.395 TL 2015 na kanuni zake za mwaka 2002. Sheria na kanuni hizo zimeweka mipaka ya wanaotakiwa kunufaika na mpango huu na wanaotajwa ni mchangiaji mwenyewe na mwenza wake, watoto wa kuwazaa, kuasili au kufikia, wazazi wa mchangiaji au wakwe zake.

Sina tatizo na sheria kwa sababu sheria ni mawazo ya watu. Walikaa wakapanga utaratibu uwe hivyo na ukapitishwa ikawa sheria. Kilichonisukuma kuandika juu ya jambo hii ni utaratibu wa mchangiaji kupangiwa wategemezi. Tatizo haliko kwenye idadi inaweza kubaki hiyo ya watu sita kama ilivyo sasa.

Lakini sheria isitamke kwamba ni nani na nani wanaotakiwa kuwa kwenye mpango huo, mchangiaji awe huru kuweka mtegemezi anayemtaka na sababu zake. Mosi, kuna wachangiaji ambao hawana watoto wao wa kuzaa pengine hawakujaaliwa watoto kabisa, mbaya zaidi wanaweza kuwa pia hawana wazazi.

Lakini watumishi hao wanalea wadogo zao wa kuzaliwa tumbo moja, wanalea watoto wa ndugu zao ambao wengine wazazi wao wamefariki, wanalea bibi na babu zao au wanafamilia wengine ambao wanawategemea kama wazazi wao.

Mfano, Juma ni mtoto wa kwanza kwenye familia, wazazi wao wamefariki dunia wote, amebaki analea wadogo zake ambao hawana msaidizi mwingine yeyote zaidi yake. Lakini sheria ya mfuko wa bima ya afya hauwatambui hao wadogo zake.

Kwa hiyo Juma anakatwa fedha kila mwezi za uanachama, anatibiwa yeye na kama ameoa na mwenza wake pekee huku akitoa tena fedha nyingi mfukoni kuwatibia nduguze.

Unajaribu kujiuliza hivi mfuko wa bima unamaana gani kwa mtumishi je, ni suala la kuleta nafuu kwake au ni suala la kuchangia tu? Na kama ni kuchangia kwa nini lisiwe suala la kila mtu ndani ya nchi lisiwe la watumishi pekee?

Nafahamu kuna hoja kwamba masuala ya bima ukichangia si lazima unufaike wewe na kwamba unachangia wasiojiweza. Hivi inaingia akilini kwamba wasiojiweza wako ndani mwako lakini sheria haiwahusu?

Ninaamini jambo hili linawaumiza sana wachangiaji ambao wengi wao wana mishahara midogo wasio na marupurupu kama ya wabunge. Wengi wao wana wategemezi wengi kutokana na kwamba wanatoka katika familia za kawaida sana.

Ni kweli kwamba idadi ya watu sita ni ndogo kutokana na aina za familia zetu za kiafrika, ukweli kwamba kila mtu kwenye familia hawezi kutibiwa na bima ya afya unajulikana, lakini idadi hiyo ndogo ya watu sita sheria isitaje nani anatakiwa kuhudumiwa suala la msingi ni kuzingatia idadi ili mtumishi aamuwe yeye anayewaona ni wahitaji zaidi kuliko sheria kuweka kizingiti kwa kutamka.

Vinginevyo naweza kuamini kwamba mpango wa bima ya afya hauna lengo la kumpa nafuu mchangiaji, badala yake itakuwa janja ya kuchukua fedha zao ili kuwalipa mishahara mikubwa watumishi wa NHIF wenyewe na kufanyia mambo mengine ambayo yako nje ya utaratibu wa huduma ya afya.

Iko hoja kwamba tukiwaruhusu wawe huru wataweka watu ambao si ndugu zao.

Hata wakiweka watu ambao si ndugu zao watu hao watakuwa Wakenya au Waganda kwani si Watanzania? Kama lengo ni kuchangia huduma za Watanzania wasiojiweza kuna shida gani hata ikitokea hivyo?

Kama mahesabu yalipigwa kwamba kwa makato haya, wanaostahili kupata huduma ni sita (6) kuna shida gani kila mtumishi akiwa na wategemezi wote sita? Je, mfuko unatumia sheria kujinufaisha? Kwa sababu kwa sheria jinsi ilivyo inawazuia wachangiaji wengi wasiwe na wategemezi wanaonufaika na Bima.

Nafikiri ni wakati mwafaka sasa marekebisho ya sheria hii yafanyike ili kuwapa uhuru wachangiaji nani wamweke kwenye mpango wa matibabu maana ndiyo wanaofahamu nani muhitaji zaidi katika familia.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mwanameka ulitumika kujibia 'pepa' skuli, ngoma za wasanii leo ukakasi*



Na Adam Fungamwango

WIKI iliyopita tulikuwa na mada yenye kichwa cha habari, 'Wasanii wataendelea kuwaponza walimu, ngoma zao hazina maadili.'

Tulizungumzia kisa kilichotokea Tunduma, Mbeya, ambapo zilisambaa video fupi zilizoonyesha wanafunzi wa shule ya msingi walicheza wimbo maarufu wa sasa wa msanii Zuchu ulitwao, 'Honey.'

Jinsi ulivyokuwa unaimbwa na kuchezwa na madenti wake, ulimwibua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda ambaye kwanza kabisa akapiga marufuku wanafunzi kucheza nyimbo zisizo na maadili na kuwataka walimu kuwa wasimamizi wa maadili pindi wanafunzi wawapo shuleni.

Halafu akaiagiza waondolewe madaraka ya ukuu wa shule watafutwe wakuu wengine wa shule.

Hata hivyo, baada ya majadiliano bungeni, walimu hao walirudishiwa vyeo vyao.

Pamoja na hayo ukweli utabaki pale pale kuwa chanzo cha yote ni wimbo huo. Na si wimbo huo tu, kwa miaka ya hivi karibuni wasanii wengi nchini hasa wa kizazi kipya wamekuwa akitunga na kutoa nyimbo ambazo kwa kweli maneno yake ni makali na yenye ukakasi, pamoja na matusi kiasi kwamba baba mwenye heshima zake hawezi kuzisikiliza mbele ya watoto wake.

Hizo video zake ndiyo kabisa ni utata mtupu. Wakati mjadala ule ukiendelea, BASATA nao wakaibuka na kumfungia miezi sita msanii Whozu na faini ya Sh. milioni 3 kwa kuchapisha video ya wimbo 'Ameyatimba', una maudhui yanayokiuka kanuni za maadili kutokana na kuwapo ishara ya vitendo vinavyoashiria matusi.

Wasanii Mbosso na Billnas ambao wameshirikishwa kwenye wimbo huo, wao wamefungiwa kutojihusisha na muziki kwa miezi mitatu na faini ya Sh. milioni 3.

Tunawapongeza BASATA, lakini kama wangekuwa makini sana, wangezifungia nyimbo nyingi mno.

Baada ya makala ile, wasomaji wengi walituma meseji na simu kupongeza na kutoa maoni mbalimbali. Wengi wao ni wazazi ambao wameonekana kutorodhishwa na nyimbo za baadhi ya wasanii wa sasa.

Mmoja akaenda mbali sana na kusema kizazi cha wasanii na wanamuziki bora kinaenda kumalizika siku hadi siku.

Akasema miaka ya katikati ya 1980, mwanamuziki Marijani Rajab walitunga wimbo unaoitwa 'Mwanameka' ambao mwaka 1990 ulichukuliwa na Baraza la Mitihani Tanzania na kuingizwa kwenye moja ya maswali fasihi ya mtihani wa Kiswahili ya kidato cha nne.

Miaka 33 imepita sasa badala ya sanaa ya muziki kwenda mbele, inarudi nyuma kutokana na wasanii wa sasa kutopenda kuumiza vichwa.

Hiki ni kizazi zilichojaliwa teknolojia ya hali ya juu, lakini kinakosa ubunifu, wakati kina Marijani wakiwa na uwezo mkubwa lakini teknolojia ilikuwa nchini.

Ni kweli kabisa inasikitisha kuona wimbo wa muziki wa dansi unachulikuwa na kutungiwa mtihani wa wanafunzi kumaliza Kidato cha Nne, miaka 33 baadaye, Waziri na wadau wengine hawataki kuona wanafunzi kucheza nyimbo zisizo na maadili wawapo shuleni.

Siwezi kukwepesha maneno kusema ni aibu kwa wanamuziki na wasanii wa sasa. Kama mimi msanii wa muziki ningejiuliza, Marijani alikuwa na nini na mimi nina nini nisiweze kuwa na tungo zitakazoishawishi angalau basi hata kuchukuliwa na kutungiwa maswali kwenye vitabu vya kiswahili, achilia mbali kuingizwa kwenye Mtihani wa Taifa.

Labda kuna watu wa vizazi vya sasa wanaweza kujiuliza Marijani aliimba kitu gani hadi mashairi ya wimbo huo yakatumika kwenye mtihani wa Kidato cha Nne.

Hebu pitia mashairi haya ndipo utagundua kuwa nchi hii walipita watu kwenye uwezo mkubwa wa utunzi na fasihi kwenye muziki, na ni shule toka kwa wasanii wa sasa kuacha nyimbo zenye maneno ya ukakasi. Tena huu ni wa mapenzi, lakini hauna chembe ya ukakasi, badala yake una fasihi, semi, tamathali, kifupi umejaa na kushiba kila kitu hadi ufasaha wa lugha ya Kiswahili.

"Kweli penzi eee, penzi lavunja undugu, watu wakakorofishana, wakakosa kusikikiliza, penzi lavunja nyumba ee, nimeyaona kwa Musa, Mwanameka umeleta maneno umeuvunja unyumba kwa Musa.

Mwanameka eee ee, Mwanameka jirani yangu, mimi naona vibaya, umemponza mama eee, umemponza mwenzio, Mwanameka umeleta maneno umeuvunja unyumba kwa Musa.

Uliposikia eee ee kwamba Musa ameona, kaoa mke wa ndoa, Musa kataka tulia ee, uhuni kaweka kando, ukatumia kila uwezo kuyabadili mawazo ya Musa.

Watambua eee ee, ukipusa mrembo, ukazidisha na mapambo, vipini wanja kwa poda ee, na mwendo wako maringo, Musa macho yake yameona na moyo ukaanza sononeka.

Ukabadili na njia eee, lazima upite kwa Musa, ukienda sokoni kwa Musa, Musa amevumilia ee, mwisho kapotea njia, kakusimamisha bila kutambua akazungumza neno la mapenzi.

Ulipopata kauli yake ukakubali bila kusita, uliyotaka yamekuwa, kazi ikawa ni moja, eee, ni mapenzi moto moto, umempa pendi lenye huda maneno matamu kama asali.

Ukichanganya na urembo wako, Musa kanasa kwenye ulimbo, akili zake zimemruka, kwako wala habaduki, kwa mkewe hakumbuki, amekwisha ionja asali anataka kuchonga mzinga.

Penzi nalo eee ee, penzi nalo halina siri na siri si ya watu wawili, mkewe Musa katambua eee, naye kadai talaka, jama Musa ameumbuka kakosa mwana na maji ya moto.

Kweli Mwanameka umefanya madhambi makubwa, mambo ulomfanyia Musa yanasikitisha.

Eee Mwanameka mkasa uliofanya ni wa mwaka, ooo bwana Musa hatokushau mpaka kufa. Tena amekwisha apa mambo ya upuuzi hataki tena, keshaumwa na nyoka akiona unyasi anashituka. Eee Mwanameka hebu punguza matata."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie kwenu-19

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

BABA akamwambia anaamini kama mtoto yuko hai basi iko siku atajitokeza na kama siku yeye akifa basi ameshaandika urithi wa mtoto huyo, akijitokeza na kuthibitika kuwa ni yeye, basi apate mgawo wake wote. Ila alifanya hivyo kwa siri bila kuiambia familia yake kwa sababu hawakutaka mtoto yeyote wa nje arithi, lakini yeye hakutaka damu yake kama iko hai iteseke."

"He! Kumbe maisha yale yote ya ufukara baba yako alikuwa tajiri? Masikini weee."

"Ni kweli Catty, ila kama nilivyokueleza, mazingira hayakuruhusu, mama aliingilia ndoa ya watu."

"Du! Ila mzee alifanya kitu cha busara sana."


"Ni kweli, ila kabla hata baba hajafariki, mzee huyo aliniambia yeye alikwenda Ulaya na huku nyuma baba akafariki dunia. Na kuchelewa kote kupata haki yangu ni kwa sababu yeye aliyepewa hati hizo hakuwapo nchini, ndiyo maana aliporejea na kukuta kifo chake, akaanza kunisaka kwa kuanza kuulizia watu taratibu hadi alinipata."

Catty alishindwa kusema lolote. Aliona kama ndoto hivi. Au hadithi za kufikirika.

"Unajua Catty sikuamini. Nikamwambia mzee siamini hilo. Akanitolea hati zote na kweli niliposoma na elimu yangu tu ya kawaida nikaamini. Lakini nikamuuliza ni kweli nitazipata wakati ndugu za baba wamenikana? Akaniambia yeye ni mwanasheria, hilo atakwenda kulisimamia mwenye mahakamani. Na baada ya hapo akaniambia kuanzia siku ile nisikae tena pale, badala yake nikakae nyumbani kwake hadi hukumu itoke kwa sababu ni hatari kwa maisha yangu kama watoto wa mzee Kamagi wakijua hilo wakaweza kutuma watu kuniua kiurahisi tu kama wakifuatilia na kugundua nikakaa pale nilipokuwa nikiishi. Ndiyo maana nikatoweka. Na sikumuaga mtu kwa sababu sikutakiwa kabisa kufanya hivyo."

"Jamani Mungu mkubwa." Catty akajikuta akiropoka kwa hisia kali na msisimko.

"Basi nikwambie Catty, nikaenda kukaa kwa hiyo mzee mwanasheria, akafungua jalada la mirathi mahakamani, watoto wote watatu wa mzee Kamagi na ndugu wakaitwa, kwanza alinikataa katakata kuwa hawanijui. Nikaiambia mahakama kuwa ushahidi huu wa maandishi nimeachiwa na mama yangu akiniambia mimi baba yangu ni nani na nini kilitokea tangu mama yangu akapewa ujauzito wangu hadi nilipofukuzwa. Nikaiambia mahakama jinsi nilivyokwenda kwao nao wakakubali kuwa tukio hilo limetokea kweli, lakini hawawezi kunijumlisha kwenye mirathi kwa sababu mimi ni mtoto wa nje ya ndoa."




**"Ni kweli, ila kabla hata baba hajafariki, mzee huyo aliniambia yeye alikwenda Ulaya na huku nyuma baba akafariki dunia. Na kuchelewa kote kupata haki yangu ni kwa sababu yeye aliyepewa hati hizo hakuwapo nchini, ndiyo maana aliporejea na kukuta kifo chake, akaanza kunisaka kwa kuanza kuulizia watu taratibu hadi aliponipata."**

"Mmmh! Halafu ikawaje?"

Mwanasheria akaja na nondo, akauweka ushahidi wote wa wosia uliandikwa kwa mkono na marehemu mwenyewe akinitambua kuwa mimi ni mtoto wake. Hakunitaja kwa jina, lakini aliandika kama alivyoandika mama. Yaani walitofautiana maeneo machache tu, na akasema kama Farida akajifungua mtoto na akawa hai hadi yeye atakapofariki, basi ajumuishwe kwenye urithi.

Wosia ukakubalika, lakini sasa ikawa kazi ya kuthibitisha kama mimi ni mtoto wa mzee Kamagi.

Bahati nzuri mama alinipa picha za baba yangu alizozichukua kabla hajafukuzwa na vitu vingine mbalimbali ambavyo vilithibitisha kuwa vilitoka kwenye nyumba ya mzee Kamagi na vilichukuliwa na mtu wa karibu ambaye ni mama yangu, ikaamriwa kwenda kupima na vinasaba, vikakabidhiwa, na baada ya kupitia kila kitu mahakama kwa kauli moja ikakubalia na hoja ya sisi wadai ikanijumuisha kwenye mirathi."

"Hongera sana James na pole, sana."

"Ahsante Catty. Haya ndiyo maisha na hii ni changamoto kwenye maisha ya mwanadamu. Baada ya hapo ikabidi ndugu zangu watekeleze kila kitu walichoamriwa na mahakama, kwa hiyo na mimi nikaingizwa nikapewa hisa kwenye kampuni za mzee Kamagi, nyumba na kusimamia baadhi ya miradi.

"Awali, ndugu zangu walichukia sana, mzee aliyenichukua yule mwanasheria akaniambia bado niendelee kukaa kwake kwa usalama, lakini kila siku zilivyodizi kusonga mbele ndugu zangu wakaanza kunielewa kutokana na kupiga kazi kama mbwa! Yaani wao wenyewe sasa wakanikabidhi nisimamie kampuni zote za mzee ili wao wapumzike na wafanye kazi zingine.

"Unajua si watoto wa mama wale wamelelewa kimayaimayai, ilikuwa inawasumbua sana, wakaajiri watu wa kuwasaidia kusimamia, lakini nilipoingia mimi walipoona napiga kazi kama mchwa, wakaona mtu si huyu, na hii si damu yetu, ngoja tumkabidhi kazi. Mapenzi kwangu yakazidi hadi leo tunaelewana na wananipenda. Ndiyo maana unaniona leo niko hapa na niko hivi." James akamaliza kuhadithia kilichotokea tangu atoweke pale mpaka siku ile aliporudi tena. Catty akamkumbatia James, huku machozi yakimtoka.

"Mungu mkubwa na aendelee kukusimamia, hali ile na manyanyaso uliokuwa ukiyapitia hadi leo uko hivi kusema kweli siamini."

"Shauri yako kama huamini." James akajibu kwa mzaha, wakaangua kicheko. Ukimya ukatawala kidogo. Wakatazamana na kutabasamu, halafu Catty akampiga swali la kizushi.

"Haya pamoja na yote hayo, umeshaoa?"

"Bado, bado sana!"

"Kwa nini wakati sasa hivi uko njema rafiki yangu? Unaniangusha!"

"Kuoa si jambo la kukurupuka, ila nitaoa kwa sababu ninaye ninayetaka kumuoa."

Catty akaguna kidogo, halafu anyooosha kidole chumbani ambako Carry amejifungia tangu alipowasili. James akaangua kicheko bila kujibu lolote.

"Basi samahani James, ngoja nitoke kidogo, nisubiri kikanunue kitoweo samaki nije niunge tule kabisa chakula cha usiku leo kabla hujaondoka."

"Haina tatizo Catty, hata mimi nitafurahi sana, maana itanikumbusha zamani sana, itanikumbusha miaka ile nilikula sana hapa nyakati nilipougua."

"Usijali." Alisema huku akitoka.

********************

"Samahani James nimekubali kuwa mke wako." Ilikuwa ni sauti ya kumbembeleza, iliyojaa simanzi ikitoka kwenye kinywa cha Carry.

Baada ya kujifungia ndani ya aibu, alijikaza na kuamua kutoka nje ili kujaribu bahati yake kwa James yule yule aliyekuwa akimsimanga, kumnyanyasa na kumnyanyapaa, akimpakia maneno makali ya dharau.

Alichukua muda ule ule ambao mdogo wake Catty amekwenda kununua kitoweo kwa ajili ya chakula kumbembeleza. Na hii ni baada ya kuona mabadiliko makubwa kwa mwanaume ambaye alikuwa akimhusudu awali, pia kusikia kila kitu alichokuwa akimsimulia mdogo wake sababu ya kuonekana sasa ana uwezo.

"Mke?" Akauliza na kushangaa James kwa wakati mmoja.

"Ndiyo." Alisema huku akipigia magoti.

"Nilipokutaka mwenzangu hukunihitaji. Ulichohitaji ni mtu mwenye uwezo, pesa au mali. Na umethibitisha hilo kwa kuniona kwa sasa niko hivi, nimebadilika." James akampa makavu Carry kwa sauti ya kujiamini.

"Ningeweza kufikiria kukukubali kama ungekuwa na angalau heshima na mimi. Ndiyo sina kitu nisingeweza kumudu kukutunza, lakini heshima yangu kama binadamu ingebaki pale pale kama alivyofanya dada yako. Ulinikataa sana, lakini kwa kunibeza, kunidharau, kunidhalilisha na kuninyanyasa. Kwa hili siwezi, kwa sababu hata nikikubali na kukaa na wewe sitoweza kusahau. Litaendelea kukaa kichwani kwangu milele hata tukiwa mke na mume." Akajibu James, Carry akiangua kilio.

"Nisamehe sana Carry kwa hilo, huna haja ya kulia, mimi nilikusamehe kitambo tu, kuwa na amani mimi si mtu wa visasi. Nitaendelea kuongea na wewe na kukusamiliana, kupiga stori popote tutakapoonana, na kukusaidia kwa chochote utakachohitaji, hata kama utataka kazi kwenye makampuni ya baba yangu aliyoyaacha, ila ambacho sitoweza ni kuwa tena mke au mpenzi wako."

"Jamani James binadamu tumeumbwa makosa, nisamehe nimekosa mwenzio."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# PENZI LIKIISHA LAWAMA

MWIGIZAJI wa Marekani, Keke Palmer amesema anatafuta ulinzi dhidi ya vitisho kutoka kwa mpenzi wake wa zamani Darius Jackson, kwa madai ya unyanyasaji wa kimwili na kihisia.

Msanii huyo mwenye umri wa miaka 30, aliwasilisha mahakamani amri ya zuio la kupata ulinzi wa kisheria na kimwili kwa mtoto wao wa miezi 8, Leodis anayejulikana kama Leo.

Katika hati za mahakama, ambazo zilipatikana zinaonyesha ukurasa wa sita, Palmer anadai kwamba kumekuwa na matukio mengi ya unyanyasaji wa kimwili" na mpenzi wake huyo Jackson (29) ambayo ni pamoja na kuharibu mali yake ya kibinafsi.

"Alitupa vitu vyangu mitaani, kutupa funguo za gari ili kunizuia nisiendeshe gari," amesema.

Katika sehemu nyingine nyaraka hizo zilieleza Jackson amempiga mbele ya mtoto wao, kumtolea maneno machafu mtoto wao na kutishia kumuua kwa bunduki ikiwa angemuacha.

"Nimenyanyaswa na kutendewa vibaya kimwili na kihisia," ameongeza.

Ingawa wapendanao hao walitengana rasmi mwezi uliopita baada ya zaidi ya miaka miwili kuishi pamoja, nyota huyo amedai kuwa katika video ya usalama za hivi majuzi zinaonyesha mwanaume huyo akiingia nyumbani kwake bila yeye kujua au ridhaa yake kisha alimtishia, akamshambulia kimwili kwa kumpiga, kumtupa juu ya kochi.

Pia mwigizaji huyo anadai mpenzi wake huyo wa zamani alichukua simu yake ili kumzuia asiwapigie simu polisi.



# Omondi sasa inatosha

MCHEKESHAJI kutoka Kenya, Eric Omondi, ameibua mjadala kwa mashabiki zake baada ya kutangaza kumkatia hati ya kusafiria mtoto wake Kaylar akiwa na umri wa wiki mbili baada ya kuzaliwa.

"Mtoto wangu ni malkia amekuwa baraka nyingi kwangu ndio maana kama baba nilihakikisha kuwa amepata pasipoti wiki mbili baada ya kuzaliwa kwani malkia anafaa kusafiri nchi zote," amesema Omondi.

Hata hivyo Omondi amesema binti yake huyo sasa amefikisha umri wa miezi mitatu, anafurahia kukua kwake hasa kutokana na urembo na upole wake.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**MADRID WAMFUNGIA KAZI HAALAND**
REAL Madrid huenda ikaamua kuipa presha Manchester City kuweka kipengele cha kumuuza mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23 msimu ujao, ambao Wahispania hao wanaamini kuwa ni karibu euro milioni 200. (***AS***)

**ANTHONY, SANCHO KUUZWA**
MARA tu uchukuaji wake wa asilimia 25 wa Manchester United utakapokamilika, Sir Jim Ratcliffe atataka kumuuza mshambuliaji Mfaransa Anthony Martial mwenye umri wa miaka 27, winga wa England, Jadon Sancho mwenye miaka 23 na winga wa Brazil Antony mwenye miaka 23. (***Mirror***)

**MAN UNITED KUMNUNUA MBAPPE**
MANCHESTER United inaweza kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 wa Paris St-Germain ukikamilika mwakani. (***Football Insider***)

**REAL MADRID NA MBAPPE**
REAL Madrid inabakia kuwa kimbilio la Kylian Mbappe endapo ataondoka PSG, lakini timu hiyo ya Hispania itakabiliwa na ushindani kutoka kwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikiwamo Manchester City, Man United Newcastle United, Chelsea na Liverpool. (***TeamTalk***)

**PAGUETA KUMRITHI DE BRUYNE**
KLABU ya Manchester City inaweza kumnunua kiungo wa kati wa West Ham raia wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 26, ambaye Kocha Pep Guardiola anamwona kama mrithi Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 32. (***UOL, via MEN***)

**DE GEA KUTUA REAL BETIS**
GOLIKIPA wa kimataifa wa Hispania na mlinda mlango wa zamani wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 33, yuko tayari kujiunga na klabu ya Real Betis ya Hispania kwa mkataba wa muda mfupi. (***El Desmarque***)

**BARCA WAMWANIA MASCARDO**
BARCELONA inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Corinthians, Gabriel Moscardo mwenye umri wa miaka 18 mbele ya Chelsea, ambaye nia yao ya kumsajili Mbrazil huyo msimu uliopita iliambulia patupu. (***90min***)


**LIVEPOOL KUMNUNUA GRAY**
LIVERPOOL inajiandaa kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United na England, Archie Gray mwenye umri wa miaka 17 ambaye anaweza kugharimu zaidi ya pauni milioni 40. (***Mail***)

**SPURS YAMKAUSHIA RADON**
LICHA ya kupunguzwa kwa chaguo lao la beki wa kati, Tottenham Hotspur haiwezi kumrejesha mlinzi wa Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 26 kutoka katika kipindi chake cha mkopo cha msimu mzima kwenye klabu ya Leeds United. (***The Athletic***)

**AL-HILAL KUMTEMA NEYMAR**
MSHAMBULIAJI wa Brazil Neymar huenda akafutiwa usajili na klabu ya Saudi Arabia Al-Hilal baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kutolewa nje msimu huu kutokana na jeraha. (***Arriyadiyah, via Goal***)

**IRANKUNDA AWANIWA BAYERN**
KLABU ya Bayern Munich inatazamiwa kushinda katika kinyang'anyiro cha kumsajili winga wa Australia, Nestory Irankunda mwenye umri wa miaka 17 kutoka Adelaide United. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAGUIRE 'AMPORA' NAMBA VARANE

**MANCHESTER,** England

**Kocha Ten Hag aweka wazi uhusiano wake mzuri na Mfaransa huyo, kiwango cha Maguire...**

ERIK ten Hag amesisitiza kuwa hakuna tatizo katika uhusiano wake na Raphaël Varane na kusema kukosa kwa Mfaransa huyo kucheza kunatokana na kiwango kizuri cha Harry Maguire.

Varane alikuwa chaguo la kwanza katikati ya safu ya ulinzi msimu uliopita lakini ametajwa kwenye benchi mechi tatu kati ya nne zilizopita za Manchester United, ikiwa ni pamoja na kipigo cha 3-0 kutoka kwa Manchester City.

Lakini alipoulizwa kama kulikuwa na tatizo na mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, Ten Hag alisema: "Hapana kabisa. Kama nilivyosema, ni kuhusu sababu za kiufundi kwa nini nilichagua ushirikiano huu. Nadhani Harry (Maguire) na Jonny (Evans) walifanya vizuri.

> **"Mwaka jana Harry hakucheza sana, kwa hiyo nilifurahishwa sana na uchezaji wa Rapha.**

Nimekuwa nikifurahishwa na uchezaji wake, lakini kwa wakati huu, Harry anacheza vizuri sana na kuna ushindani wa ndani."

Evans alikosa mechi ya Ligi Kuu ya England dhidi ya Luton Town Uwanja wa Old Trafford jana, huku United ikithibitisha Ijumaa kwamba beki huyo wa Ireland Kaskazini "atakuwa nje ya uwanja kwa wiki chache zijazo" baada ya kusumbuliwa na paja.

Kutokuwapo kwake kunamuacha Ten Hag kuchagua kati ya Varane, Maguire na Victor Lindelöf. Varane na Maguire walicheza pamoja wakati wa kichapo cha 4-3 dhidi ya FC Copenhagen Jumatano baada ya Evans kubadilishwa lakini Ten Hag alidokeza kuwa wao si washirika bora nyuma.

"Kuna nyakati katika michezo fulani ambapo wanaweza kucheza pamoja na tayari wamethibitisha kuwa wanaweza kufanya hivyo," alisema kocha huyo.

"Lakini hali ya kujijenga haiko hivyo wakati mmoja wao anacheza kutoka nafasi ya beki wa kati wa kushoto kwa sababu nadhani Lisandro Martínez, Luke Shaw, Jonny Evans na Victor Lindelof, wana mguu wa kulia, lakini wanaweza kucheza kwa raha na kushoto kwao na kutengeneza pembe za kulia, kisha unaweza kuunda muundo bora ambapo unaweza kuanza kucheza."

Kikosi cha Ten Hag kimeruhusu mabao 30 katika michezo 17 na 10 katika mechi nne zilizopita.

Mholanzi huyo amesema orodha ndefu ya majeruhi imechangia lakini amekiri kwamba wachezaji wake wanaopatikana wanapaswa kufanya vizuri zaidi."

"Tulikuwa na kipa mpya anayeingia na kila unapounda beki wanne na wanajua sheria na kanuni, lakini taratibu hazifanani.

"Mawasiliano ni muhimu sana, lakini hayo yote ni maamuzi ya kugawanyika. Unahitaji ushirikiano huo na unahitaji kwa asilimia 100 kwa sababu yasipofanya kazi, basi unaruhusu mabao katika kiwango hiki.

"Hadi sasa, nadhani tusingeweza kucheza kikosi cha kwanza nilichotaka. Lakini hiyo kamwe si kisingizio. Tunataka kushinda michezo na tuna wachezaji wazuri katika kikosi na wote wanaweza kufanya kazi."

# MAJERUHI YAIPASUA KICHWA SPURS



**LONDON,** England

ANGE Postecoglou amesema Tottenham Hotspur "haitamudu majeruhi tena" baada ya kuthibitisha kuwa Micky van de Ven na James Maddison hawatacheza tena mwaka huu 2023.

Van de Ven alipata jeraha la msuli wa paja muda mfupi kabla ya Maddison kuchechemea kutokana na tatizo la kifundo cha mguu wakati wa mechi ya Jumatatu waliyochapwa 4-1nyumbani na Chelsea.

Hapo awali Maddison alikuwa ameitwa kwenye kikosi cha hivi punde zaidi cha kocha Gareth Southgate cha England lakini akajiondoa Ijumaa asubuhi huku ukubwa wa tatizo hilo ukidhihirika.

Akizungumza kabla ya safari ya Jumamosi kwenda kwa Wolves, Postecoglou alielezea matatizo yanayoongezeka ya utimamu wa viungo vya timu yake na kuthibitisha kuwa Richarlison naye amefanyiwa upasuaji wa nyonga.

"Micky ana jeraha la misuli ya paja ambalo tulijua," alisema Postecoglou. "Labda miezi michache kwake, akiangalia mwaka mpya.

"Maddison hali yake ni mbaya zaidi kuliko tulivyofikiria. Ni wazi kwamba alitoka na jeraha la kifundo cha mguu lakini siku iliyofuata hakuwa mzuri kwa hivyo tulimpeleka kufanyiwa tena uchunguzi zaidi na hataweza tena kucheza mwaka huu.

"Richy alikuwa na upasuaji ambao tulipanga kwa sababu amekuwa akipambana nao tangu siku ya kwanza na wakati mapumziko ya kimataifa yanakaribia, tuliona ni wakati mzuri wa kuifanya. Anapaswa kuwa nje kwa mwezi tu ikiwa kila kitu kitaenda sawa.

"Tunafahamu kwamba itabidi tufanye mabadiliko lakini vijana wanaoingia wamekuwa wakifanya mazoezi kwa bidii na kuelewa jinsi tunavyotaka kucheza.

"Najua watu wamesema imekuwa faida kwamba hatujakuwa kwenye michuano ya Ulaya au lakini kama tungekuwa, baadhi ya watu hawa wangekuwa na wakati wa kucheza. Hilo ni suala gumu.

Kwa mtazamo wetu, hatuwezi kumudu majeruhi zaidi, lazima tuwe waangalifu kuhusu aina ya muda wa mchezo tunaowapa watu."

Akitafakari jeraha la Van de Ven, Postecoglou alitaja kukosekana kwa Destiny Udogie na Cristian Romero, ambao wote watasimamishwa kucheza Molineux baada ya kupewa kadi nyekundu dhidi ya Chelsea.

"Kutokuwapo kwao kuna athari timu," alisema. "Ile isiyo ya kawaida kwetu, tumewapoteza watatu nyuma ya wanne.

"Hapo ndipo tunapoathirika zaidi kuliko kitu kingine chochote. Kama ni Micky tu, isingetuvuruga sana lakini wachezaji watatu tofauti nyuma ya nne na hiyo ndiyo changamoto kubwa kwetu."

## Man City yafufua mpango kumsajili Paqueta

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inataka kurejea kwenye meza ya mazungumzo kwa ajili ya kiungo wa West Ham, Lucas Paquetá, kwa mujibu wa UOL.

Man City wamekubali mkataba wenye thamani ya pauni milioni 80 kwa kanuni kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 msimu wa joto, lakini hawakukamilisha uhamisho huo baada ya kubainika kuwa alikuwa akichunguzwa kwa madai ya uvunjaji wa sheria za kamari.

Hata hivyo, ripoti za hivi punde zinaonesha Man City "wamedhamiria" kutoa ofa mpya ya kuinasa saini yake Januari kama wanaweza kupata ufafanuzi kuhusu hali yake.

Kocha Pep Guardiola anaripotiwa kumuona Paqueta kama mrithi wa muda mrefu wa Kevin De Bruyne, ambaye anatazamiwa kumaliza mkataba wake na Man City mnamo 2025, pia amekuwa akipambana na tatizo la misuli ya paja msimu huu.



Paqueta amesalia kuwa mchezaji muhimu wa West Ham katika kampeni ya sasa, akiwa amecheza mechi 15 katika mashindano yote kwa kikosi cha kocha David Moyes, alifunga bao la ushindi wakati wagonga nyundo hao wakiilaza Olympiacos 1-0 kwenye Ligi ya Europa Alhamisi.

# Alvarez afurahia kucheza na Messi, Haaland




**MANCHESTER,** England

JULIAN Álvarez ameiambia ESPN kwamba ni "ndoto" kucheza pamoja na Erling Haaland pale Manchester City na Lionel Messi akiwa na Argentina baada ya kuweka historia na klabu na nchi msimu wa 2022-23.

Álvarez amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA, na pia kubeba Kombe la Dunia mwaka huo huo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alisema kuwa fursa ya kusugua mabega na kujifunza kutoka kwa wachezaji hao wawili bora katika mchezo huo ni kitu anachothamini.

"Kucheza na walio bora zaidi na kufanya mazoezi na walio bora zaidi hukufanya kuwa bora na kujifunza mengi," alisema Álvarez katika mahojiano na ESPN.

"Ni ndoto kubwa miongoni mwao na kukua kama mchezaji na mtu."

Fowadi huyo wa Argentina alifunga mabao 17 katika kampeni yake ya kwanza akiwa na City na tayari amefunga mara saba na kutengeneza mabao matano zaidi katika mechi 17 alizoichezea klabu hiyo msimu huu.

"Msimu uliopita ulikuwa mrefu na mkali sana, na michezo mingi," Álvarez alisema.

"Ninajisikia vizuri na ninajiamini. Nimecheza michezo mingi, dakika nyingi.

"Baada ya kuwa na dakika zaidi na tayari ni msimu mmoja hapa, mtu hujifunza mengi kutoka kwa wachezaji wenzake, kutokana na kuwasikiliza na timu ya makocha."

Álvarez anaamini kuwa City wako katika nafasi nzuri ya kuongeza taji katika kabati lao la mataji msimu huu.

"Tuko juu kwenye Ligi Kuu na kwenye Ligi ya Mabingwa tuko kamili," alisema.

"Tumekuwa na majeruhi wachache katika miezi michache ya kwanza ya msimu lakini timu inaendelea na kucheza michezo mizuri.

"Klabu hii inakuhitaji upambane katika kila nyanja. Kwa bahati nzuri, tunafanya vyema kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa. Tunaendelea kwenye Kombe la FA."

Hata hivyo, Álvarez alikiri kwamba itakuwa vigumu kwa City kufikia ushujaa wao wa kampeni za mwaka jana.

"Baada ya kushinda kila kitu msimu uliopita, kila timu itacheza na sisi kwa tofauti tukijua wakijua sisi ni mabingwa," alisema fowadi huyo wa zamani wa River Plate.

"Tunafahamu hili na hilo linatuweka katika tahadhari."

HABARI MICHEZO

## Yanga yaongoza takwimu

INATOKA UK. 24

zinafuatia kushinda mechi nyingi, wakipata ushindi mara sita kila moja, huku pia zikipoteza mara moja kama Yanga na zote kutoka sare moja moja.

Azam inafuatia kuwa timu iliyofunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu ikipachika mabao 19, Simba ikiwa ya tatu ikifunga mabao 18.

Kagera Sugar na Tabora United zinaifuatia Yanga zikiwa timu zilizofungwa mabao machache kwenye Ligi Kuu, zikiruhusu mabao saba tu kwenye wavu wao, huku Azam na Tabora United zikishika nafasi ya pili kuwa na 'clean sheets' tano kila moja.

Mtibwa Sugar ndiyo timu iliyopoteza mechi nyingi, ikifungwa mechi sita, na kufungwa mabao mengi mpaka sasa (16).

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameanza kuwafuatilia wapinzani wao kwenye kundi lao la Ligi ya Mabingwa Afrika, CR Belouizdad ya Algeria watakaoanza nao mchezo wa kwanza hatua ya makundi.

Gamondi amesema baada ya mchezo wao na Coastal Union alianza kufanya maandalizi ya programu ya kikosi chake kwa ajili ya mchezo huo wa ugenini dhidi ya miamba hiyo ya Algeria.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema wakati baadhi ya wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu za Taifa wakiendelea na programu maalum ya kuelekea kwenye mchezo, benchi la ufundi nalo limeanza kuifuatilia timu hiyo kubaini uchezaji wao.

"Kila mechi imekuwa na maandalizi yake baada ya kupata matokeo mazuri katika michezo miwili ya ligi na sasa kuna mapumziko mafupi baada ya ligi kusimama na kupisha kalenda ya FIFA kwa timu za taifa, tutatumia pia muda huu kuwafuatilia wapinzani wetu tutakaoanza nao michezo ya hatua ya makundi, lengo tunataka kuona tunaanza vizuri hatua hii," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa amewafuatilia CR Belouizdad katika michezo yao ya ligi ambapo juzi walipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya USM Alger na wanatarajia kucheza mechi mbili kabla ya kukutana na Yanga.

## Simba yawatuliza wanachama

INATOKA UK. 24

cha mabao 5-1 kutoka kwa watani zao wa jadi Yanga Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Alisema kwa sasa wapo katika hatua za mwisho kumtangaza kocha huyo, ambapo tetesi zinasema kocha wa zamani wa timu hiyo, Mbelgiji, Sven Vandenbroeck, kocha wa zamani wa Yanga, Nasreddine Nabi na Julien Chevalier ambaye ni kocha wa Asec Mimosas wote wanatajwa kuwania nafasi hiyo.

# TANZANITE KUSAKA USHINDI KWA NIGERIA LEO

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake ya U-20 'Tanzanite', leo kinashuka dimbani kusaka ushindi katika mchezo wa kwanza wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Nigeria.

Tanzanite inatupa karata yake katika mchezo huo kwenye Uwanja wa Azam, uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam, kutafuta ushindi kabla ya marudiano wiki mbili zijazo nchini Nigeria.

**Tayari kikosi cha Nigeria kimetua nchini alfajiri ya kuamkia jana tayari kwa mchezo huo muhimu wa kufuzu fainali hizo za dunia.**

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema maandalizi yameenda vizuri na kuna baadhi ya wachezaji wa JKT Queens waliopo Ivory Coast katika ligi ya mabingwa wamejiunga na timu hiyo tayari kwa mchezo wa leo.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao lakini anaimani ya kufanya vizuri kulingana na maandalizi waliyofanya kuelekea kwenye mchezo huo.

"Tuna matumaini ya kufanya vizuri kulingana na maandalizi tuliyofanya, tutacheza mchezo huo kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu wapinzani wetu kwa sababu hata wao wamejiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri," alisema Shime.

Aliongeza kuwa matarajio yao ni kuanza vizuri kwa kupata matokeo yenye faida kwao kabla ya kuelekea Nigeria kwenye mchezo wa marudiano.

"Tunaanza kucheza nyumbani, sasa kwa sababu ni mtoano ni lazima tuutumie vizuri uwanjani wa nyumbani na ikiwezekana mechi tuimalize hapa, hayo ndio matamanio yetu kama timu, lakini mpira ni mchezo wa dakika 90 tusubiri tuone tutavuna nini," alisema Shime.



Mtoto Said Ali (kulia) kutoka kituo cha michezo cha Rova Faya, akimiliki mpira huku akizongwa na wenzake wa Timu ya River Boy Academy, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKU haishikiki Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KLABU ya soka ya JKU imeendeleza ubabe kwenye Ligi Kuu visiwani humo baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mlandege na hivyo kukoleza mbio zao za kusaka ubingwa msimu huu.

JKU SC imefanikiwa kupata alama hizo tatu muhimu zinazozidi kuwaweka juu ya msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16 kwa kufikisha pointi 23 baada ya kucheza michezo 10.

Katika mchezo huo wa juzi uliochezwa kwenye uwanja wa Mau A, magoli ya JKU yalifungwa na nyota wake Salehe Kalabaka dakika ya 15 na Gamba Iddi dakika ya 28 wakati goli la Mlandege FC lilifungwa na Mussa Hassan dakika ya 67.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali, alisema kupata ushindi huo ni mwendelezo wa malengo yao kuhakikisha mpaka wanamaliza mzunguko wa kwanza timu hiyo iendelee kubaki kileleni katika msimamo wa ligi hiyo.

Alisema michezo mitano iliyobakia katika mzunguko huu wa kwanza matarajio yake makubwa ni kuona anapata alama tatu kwa kila mchezo atakaoshuka dimbani.

Alisema bado wapo katika mbio za ubingwa ambapo hawahitaji kufanya makosa katika michezo yao yote ili mwisho wa msimu kuhakikisha wanatimiza lengo lao.

"Bado tupo katika kuhakikisha hatutoki katika mbio hizi za ubingwa ndio maana mchezo wowote tunaocheza kwetu sisi ni muhimu kuhakikisha tunapata alama tatu, kikubwa wachezaji wangu waendelee kucheza kwa hamasa kama ilivyo sasa," alisema Ali.

Aidha, akiuzungumzia mchezo wao dhidi ya Mlandege, Ali alisema mchezo huo ulikuwa mgumu hasa kipindi cha pili ambapo Mlandege walimiliki zaidi mpira kwa asilimia kubwa.

Alisema kupata magoli ya mapema kipindi cha kwanza hii iliwafanya wapinzani wao wacheze kwa hari kubwa lakini bahati ilikuwa upande wao.

Ligi hiyo itaendelea tena leo kukamilisha mzunguko wa 10 ambapo michezo miwili itachezwa, katika uwanja wa Mau A, Zimamoto SC itawakaribisha wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi SC na katika uwanja wa Mau B, Ngome FC itaumana na Mafunzo SC michezo yote itachezwa saa kumi jioni.

Michezo

Jumapili Novemba 12, 2023

Nipashe

UKURASA 22



## Majeruhi yaipasua kichwa Spurs

# Yanga SC yaongoza takwimu Ligi Kuu

## ●●● Gamondi aanza mikakati kuwakabili CR Belouizdad Ligi ya Mabingwa Afrika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikisimama kwenye raundi ya tisa kupisha michezo ya kimataifa, kikosi cha Yanga kinaongoza kwa takwimu kwenye maeneo mengi mpaka sasa.

Yanga wanaongoza kwa kuwa timu yenye pointi nyingi kwenye Ligi Kuu ikifikisha pointi 24, inaongoza kwa kushinda mechi nyingi ikishinda michezo nane, lakini ndio timu iliyopoteza mechi chache, ikipoteza mechi moja dhidi ya Ihefu.

Takwimu nyingine inayoongoza Yanga ni kuwa timu pekee isiyo na sare katika michezo tisa iliyocheza ikiwazidi watani zao Simba ambao wenyewe wamepoteza mchezo mmoja na kutoa sare mchezo mmoja.

Yanga pia ndio timu yenye mabao mengi ya kufunga ikiwa na mabao 26 na kuwa timu iliyofungwa mabao machache zaidi, ikifungwa mabao matano tu huku ikiwa na Clean Sheets nyingi zaidi (6).

Wakati hiyo ikiwa upande wa timu, kiungo mshambuliaji wake, Aziz Ki, raia wa Burkina Faso na Mkongomani, Nzengeli, wanaongoza kwa kupachika mabao wakiwa na mabao saba kila mmoja, wakiwa juu ya msimamo pamoja na mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke.

Beki wa kulia wa timu hiyo, Kouassi, anaongoza kwa 'assist' akiwa ameshatoa pasi tano za mabao.

Mfululizo wa takwimu hizo zinaonyesha kuwa Yanga imekuwa tishio kwenye Ligi Kuu hadi raundi ya tisa ambapo kwa sasa ligi imesimama kupisha mechi za kimataifa.

Simba na Azam zina takwimu nyingi zinazofanana, lakini zinazofuatia kuwa na pointi nyingi, zikiwa zimefikisha 19, pia zote mbili

INAENDELEA UK. 23



Golikipa wa Simba, Aishi Manula, akiwasili kwenye kambi ya Timu ya Taifa 'Taifa Stars' jijini Dar es Salaam, kujiandaa na michezo ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Niger na Morocco itakayochezwa Novemba 18 na 21. **PICHA: BINZUBERY**

## Simba yawatuliza wanachama, mashabiki wake

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutulia, ikisema huu si wakati wa kunyoosheana vidole kwa sababu Ligi Kuu bado mbichi na hata mechi za makundi za Ligi ya Mabingwa Afrika bado hazijaanza, ambapo imeahidi kurekebisha kasoro zote zinazotajwa kuwapo.

Akizungumza jana akiwa jijini Dodoma, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wanachama na mashabiki wasicheze ngoma wasiyoijua badala yake kuwapa nafasi viongozi kurekebisha makosa.

Alisema kuwa klabu zote kubwa duniani zimepitia hatua hiyo wanayoipitia wao (Simba) saa hivi.

"Ningependa kuchukua nafasi hii kuongea na wanachama na mashabiki wa Simba kwa sababu wamehamaki na kukasirika kweli kweli..., ni kweli kwa aina ya matokeo ambayo tumeyapata hakuna mtu wa Simba ambaye yanaweza kumfurahisha, kila mtu amechukia, lakini waache vurugu, kejeli na matusi ambayo wanayatoa kwa viongozi wetu, si mienendo na tabia za Simba ni kweli tumevurugwa lakini ni lazima tuwe watulivu, ni vyema tuwe na subira ili viongozi wapate muda wa kufanya yaliyo sahihi kwa kuiboresha Simba yetu, tukianza leo huyu atoke huyu, ametuhujumu, huyu vile ina maana tunatengeneza mpasuko mkubwa," alisema Ahmed.

Aidha, alisema bado hawajapotea kwenye ramani ya ubingwa kwa kuwa ligi bado mbichi hivyo wana muda wa kurekebisha mambo na kurejea kwenye mstari.

"Hatujapotea, ligi bado mbichi, Ligi ya Mabingwa ngazi ya makundi haijaanza kwa hiyo wanasimba tutulie, tutakaa sawa tu," alisema Ahmed.

Wakati huo huo, Ahmed, alisema uongozi wa klabu hiyo unatarajia wakati wowote kuanzia kesho Jumatatu kumtangaza kocha wake mpya atakayechukua nafasi iliyoachwa wazi wa Roberto Oliveira 'Robertinho' aliyeonyeshwa mlango wa kutokea, mara baada ya kipigo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >